# Nipashe

Jumanne Aprili 12, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580913

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US



SportPesa

TZS. 1,144,195,580


BET LEO UWE BILIONEA

SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#




**Tanzania** yatajwa kuwa na mabadiliko uhuru wa kujieleza

UKURASA 3






# Mkakati kukabili makali ya maisha

• **Waziri** Mwigulu adokeza kupunguza kodi...*Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO


UKURASA WA 4

**MKENDA: ELIMU YA JUU INAPOROMOKA**

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema elimu ya juu inaporomoka huku akishangaa...

UKURASA WA 4

**KUNYONGWA HADI KUFA KWA MAUAJI**

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dodoma, imemhukumu fundi ujenzi Menruf January Haule (42) kunyongwa hadi...

UKURASA WA 7

**DAR, TANGA ZAZOROTA ANWANI ZA MAKAZI**

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema operesheni ya uwekaji wa...


## Mbunge ataka kibano zaidi Sheria ya Kujamiiana

UKURASA 3




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (katikati) akibonyeza kitufe kuashiria uzinduzi rasmi wa huduma ya teleza kidijitali iliyo zinduliwa jana na benki ya NMB, kampeni hiyo ni muunganiko wa huduma tatu ambazo ni Mshiko Fasta, NMB Pesa Wakala na malipo ya huduma kwa kutumia QR code. Kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya benki hiyo, Dk Edwin Mhede na kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu, Ruth Zaipuna na kulia ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Chande. **Habari ukurasa 8. PICHA: MPIGAPICHA WETU**



# Meya afunguka baada ya kung'olewa kazini

UKURASA 2


**MICHEZO** | **YANGA YAWALILIA AUCHO, FEI TOTO** UK.24 | **MAONI, KATUNI** UK.6



Rais Samia Suluhu Hassan, akizungumza na Waziri wa Mambo ya Nje wa Shirikisho la Jamhuri ya Ujerumani Katja Keul mara baada ya kuwasili Ikulu Jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# Serikali kupunguza kodi bidhaa

**Na Waandishi Wetu**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Mwigulu Nchemba, amesema serikali itapunguza kodi kwa bidhaa zinazoingia nchini ili kumpunguzia mwananchi mzigo wa kupanda bei ikiwa ni agizo la Rais Samia Suluhu za kuchukua hatua za muda mfupi za kukabiliana na tatizo hilo.

Waziri Nchemba aliyasema hayo jana, jijini Dar es Salaam, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kuhusu hali ya uchumi na kupanda bei ya bidhaa nchini unaotokana na majanga ya mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 na vita kati ya Urusi na Ukraine.

**KODI YA SUKARI KUSHUKA**

"Mheshimiwa Rais ametuagiza tuchukue hatua za muda mfupi huku tukiendelea kufanya monitoring (kufuatilia) tukiliangalia hili jambo linaendeleaje kwa sababu pia hakuna anayeweza kukadiria linaishaje, jambo la Covid hakuna anayeweza kukadiria na hili linaishaje linaloendelea kule la mzozo."

"Hatua za haraka kwanza sukari itakayoingia ambayo imeshaagizwa tutapunguza rate (kiwango) yake ya kodi hakitokuwa chini ya asilimia 10, tutapunguza kwa asilimia 10 kwenda juu kwa muda mfupi huu wa sasa hivi, ili kuishusha kidogo makali yake," alisema Waziri Nchemba.

Alisema ifikapo mwezi Juni wakati wanapopitisha bajeti mpya, watajua hatua nyingine ya kuchukua baada ya kuona mwelekeo wa hali ya kiuchumi ya kidunia na ndani ya nchi inakwendaje.

Vile vile, alisema punguzo hilo pia litakuwapo katika upande wa mafuta ya magari na ofisi za serikali zitaangalia namna ya kupunguza makato ili kumpunguzia gharama mwananchi.

**MAFUTA YA KULA**

Alisema, wamewaelekeza Mamlaka ya Mapato (TRA), ambao wanaangalia hatua za muda mfupi za kuchukua na baada ya mwezi mmoja na nusu wataweka viwango vipya ambavyo vitaruhusu kupunguza gharama.

Alisema pia serikali itapunguza sehemu ya gharama iliyokuwa inaongezeka kwenye vyombo vya usafiri, na baadaye watafanya tathmini ili wapunguze kwenye vifaa hivyo ikiwamo matrela wakiamini punguzo hilo litachangia kushuka kwa gharama za bidhaa.

Alisema kuwa pamoja nchi kupitia changamoto za kiuchumi na kupanda kwa bei za bidhaa zinazosababishwa na vita ya Urusi na Ukraine na UVIKO-19, shughuli za maendeleo lazima ziendelee ili kutengeneza uhimilivu wa kiuchumi.

**UPANDAJI BIDHAA HOLELA**

Katika kudhibiti kupanda kwa bei ya bidhaa kiholela, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji alisema, serikali imewaagiza watendaji katika viwanda vinavyozalisha sukari na saruji kuacha urasimu katika kutoa bidhaa hizo ili kuondoa tatizo linalotokana na uhaba wa bidhaa hizo ikiwamo kupanda bei.

Alisema pia imeziagiza mamlaka zilizopewa dhamana ya kusimamia miendendo ya soko la bidhaa ziendelee kutekeleza wajibu wao bila kumuumiza yeyote katika pande mbili ili kudhibiti vitendo vya upandishaji bei ya bidhaa kiholela hasa zinazozalishwa ndani ya nchi.

Alisema taifa limeathirika kupanda kwa bei za ngano, mafuta ya kula, mbolea na mafuta ya vyombo vya moto ya taa kwa sababu ilikuwa ikiagiza bidhaa hizo moja kwa moja kutoka nchi za Ukraine na Urusi ambazo zipo kwenye vita kwa sasa.

Kwa upande wa mafuta alisema uhitaji kwa mwaka ni tani 650,000 kwa mwaka huku ina uwezo wa kuazalisha ni tani 270,000 pekee. Wakati uhitaji wa mbolea ni tani 700,000 kwa mwaka uwezo wa kuzalisha ni 300,000.

Alisema matokeo ya tathmini ya bei za bidhaa yanaonyesha kuwa bei ya bidhaa zinazozalishwa nchini ina uhimilivu ikilinganishwa na bidhaa zinazoagizwa kutoka nje, japo zipo chache ambazo bei zake zilikuwa si himilivu ikiwamo saruji na nondo.

**MAPENDEKEZO YA ACT-WAZALENDO**

Chama hicho kimeishauri serikali kubana matumizi ili kukabiliana na mfumuko wa bei za bidhaa ikiwamo mafuta ya petroli na dizeli.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mkoani Dar es Salaam, Msemaji wa kisekta wa ACT-Wazalendo, Dorothy Semu, alisema hotuba ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, bungeni kuhusu suala la mfumuko wa bei za bidhaa halikupewa uzito kwa kuwa walitarajia kuona inatoa suluhu ya tatizo la kiuchumi, jamii na siasa linalolikabili taifa kwa sasa.

Alisema vilio kila kona ya nchi vinaashiria ugumu wa maisha kwa wananchi wengi, huku gharama zikiwa kubwa kutokana na kupanda kwa bei za bidhaa muhimu za chakula hususani ngano, mchele na mafuta ya kula, ambayo vimepanda kwa asilimia 60 hadi 180.

"Unawezaje kutoa mabilioni ya fedha kununua ndege katika mazingira ambayo wananchi hawawezi kukabili bei ya sukari, mafuta ya kula, mchele, Maharagwe na ngano? ACT-Wazalendo inaelekeza kwa serikali kuwa ni lazima ifunge mikanda kwa matumizi yake na itoe nafuu kwa jamii kwa kupunguza kodi zake angalau Sh. 500 kwa lita moja ya mafuta ya dizeli ili kuwahami wananchi," alisema Dorothy.

***Imeandikwa na Jeniffer Gilla, Christina Mwakangale na Maulid Mbaga**

# Meya afunguka baada ya kung'olewa kazini

**Na Mary Mosha,** MOSHI

ALIYEKUWA Meya wa Manispaa ya Moshi, Juma Rahibu, amefunguka baada ya kung'olewa katika nafasi hiyo na Baraza la Madiwani kwa tuhuma mbalimbali ikiwamo matumizi mabaya ya madaraka.

Baada ya uamuzi huo, Meya huyo aliyefika kikaoni kwa gari la Manispaa majira ya saa 09:37:08 asubuhi, aliondoka saa 6:21 mchana kwa pikipiki aina ya Toyo.

Katika 'status' yake ya WhatsaApp, aliandika "Siku zote ukisimama kwenye ukweli na haki huwezi baki salama. Nimejitahidi kadiri ya uwezo wangu kwenye jamii viongozi wa CCM wilaya na mkoa wamekuwa chanzo kikubwa cha mgogoro hadi hata kutisha wajumbe ili nitolewe madarakani kwa maslahi yao, Mungu ni mwema niko salama sana kazi iendelee."

Pia, katika ujumbe mwingine aliandika saa 6:12 mchana "Rasmi leo mimi sio Meya wa Manispaa ya Moshi, Mungu awajalie wote tulioshirikiana katika mambo yote."

Madiwani 28 katika Baraza Maalum la Madiwani walipiga kura ya kutokuwa na imani naye baada ya kupokea ripoti ya uchunguzi, kwenye kikao kilichofanyika kwa saa 2:53:07, kati yao 18 walitaka ang'atuke na 10 walitaka abaki.

Moja ya tuhuma zilizokuwa zikimkabili ni kushiriki sherehe ya kuzaliwa kwa kijana anayedaiwa kushiriki mapenzi ya jinsia moja (shoga), pamoja na kutumia nafasi yake ya uongozi vibaya ikiwamo kutoheshimu madiwani wenzake.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Rashid Gembe, alisema Machi 17, mwaka huu, ofisi yake ilipokea barua kutoka kwa madiwani 20 kati ya 30 wakitaka kuitishwa mkutano maalum wa kumuondoa, alimtaarifu kuhusu nia hiyo pamoja na tuhuma dhidi yake akimtaka kujibu ndani ya siku tano.

Alisema Meya Rahibu aliwasilisha utetezi uliowasilishwa kwa Mkuu wa mkoa ambaye aliunda kamati ya uchunguzi na kuwasilisha taarifa kwa Mkurugenzi.

Kamati hiyo ilichunguza kama Meya anatumia nafasi yake vibaya na kutoa maamuzi ambayo hayajapitishwa na Baraza la Madiwani, kutowaheshimu viongozi wanaohudhuria vikao, mikutano ya halmashauri, kushiriki kwenye rushwa katika usimamizi wa ujenzi holela eneo la katikati ya mji (CBD).

Mengine ni mwenendo mbaya au ukosefu wa adabu dhidi ya madiwani anaowaongoza, tabia na mwenendo wa Meya huyo kwenye jamii kwa kuhusisha nafasi na wadhifa wake kutokana na tuhuma zilizotolewa na wananchi na baadhi ya vyombo vya habari kuwa alishiriki sherehe za kuzaliwa mmoja wa kijana anayejihusisha na mahusiano ya jinsia moja na kulishwa keki.

Gembe alisema kamati ilibaini kuwa Mstahiki Meya anatumia madaraka yake vibaya na kutowaheshimu viongozi waliohudhuria vikao, anakiuka mwongozo wa mwaka 2016 uliotolewa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Nyingine ni Meya huyo kutoruhusu mjadala katika kamati ya fedha na utawala ambacho kilitakiwa kujadili suala la vikundi vilivyoomba na kupatiwa mikopo.

Kuhusu tuhuma za kubadili maamuzi ya kutoa fedha za ujenzi wa jengo la mama na mtoto katika kata ya Kaloleni, muktasari hauonyeshi mahali halmashauri iliridhia kuhamisha matumizi ya fedha hizo kwenda kujenga kichomea taka katika Kituo cha Afya Pasua kilichopo Kata ya Bomambuzi.

Alisema pia walibaini alihusika kupokea rushwa ili kuruhusu ujenzi katika maeneo ya katikati ya mji na yeye (Meya) kukiri hivyo katika kikao cha kamati ya siasa ya wilaya.

Mkurugenzi Gembe akinukuu taarifa ya kamati hiyo alisema kuwa "Yapo mambo yanayofanywa na Mstahiki Meya yanayoonyesha kuwa ana mwenendo mbaya na ukosefu wa adabu dhidi ya madiwani anaowaongoza, ikiwa ni pamoja na kutoa kauli ya kuwatambia madiwani wenzake kwamba yeye (Meya) ni mteule wa Kamati Kuu ya CCM Taifa na kwamba hakupendekezwa na CCM wilaya wala mkoa katika nafasi ya Umeya."

Alisema taarifa hiyo ilisema mara nyingi akiwaita madiwani wenzake hawajui kitu mara kwa mara huchelewa kwenye vikao kabla ya baraza na akifika haombi radhi wenzake kwa kuchelewa pamoja na kutomkaimisha ofisi Naibu Meya na kutomruhusu kuendesha vikao kwa niaba yake anapokuwa nje ya ofisi.

Kuhusu sherehe, "Timu imebaini kuwa Mstahiki Meya alishiriki katika sherehe ya kuzaliwa kijana anayetuhumiwa kujihusisha na mahusiano ya mapenzi ya jinsia moja, alikiri (Meya) kushiriki kwa utetezi kwamba mwaliko huo uliletwa kwake kama Juma Rahibu na sio kama Meya."

Aliendelea kudai kuwa, "Hakwenda kushiriki sherehe hizo kwa mamlaka aliyonayo kwani hakutumia gari la halmashauri wala kuvaa mkufu wa mamlaka ya Umeya na katika utetezi wake wa maandishi alieleza kuwa suala hilo kuendelea kujadili linachochea ubaguzi dhidi ya makundi flani katika jamii na kutaka kuharibu tunu ya taifa, uhuru na umoja."

Aidha, Mkurugenzi huyo alisema timu ya uchunguzi imethibitisha Mstahiki Meya alishiriki katika sherehe husika na tukio hilo halionyeshi taswira nzuri kwa jamii anayoiongoza na ni kinyume cha maadili ya madiwani, utamaduni, mila na desturi za nchi.

Baada ya kura hizo Rahibu alitangazwa kuondolewa kwenye nafasi hiyo na nafasi yake kushikiliwa kwa kipindi cha mpito na Naibu Meya, Stauti.

HABARI KITAIFA

# Mbunge: Wanaonajisi watoto wahasiwe

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

Wakati Bupe akilalama kuhusu matuta barabarani, Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko , amesisitiza tena kuhusu hoja yake ya Novemba mwaka jana bungeni, kwamba kutokana na kushamiri kwa matukio ya ukatili dhidi ya watoto, anafikiria kuwa wanaobainika kufanya hivyo wahasiwe ili kuifanya jamii ya kitanzania kuwa salama.

Akichangia mjadala huo bungeni jana, mbunge huyo alisema kuna haja serikali kufanya marekebisho ya sheria ili kuwe na adhabu kali zaidi dhidi ya wanaonajisi watoto, mojawapo ni kuhakikisha wanaopatikana na hatia wanahasiwa ili kuwa fundisho kwa wengine wenye nia ya kutenda makosa kama hayo.

Jumatano ya wiki iliyopita, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, aliliambia Bunge matukio 27,838 ya vitendo vya ukatili nchini yameripotiwa kwenye vituo vya polisi nchini katika miaka minne iliyopita.

Katika matukio hayo vitendo vya ubakaji vimekithiri kwa kuwa na matukio 19,726, huku akifafanua kuwa kuanzia mwaka 2019 hadi Machi, 2022, kulikuwa na matuko ya ubakaji 19,726, kulawiti 3,260 yaliyotendwa dhidi ya wanaume 3,077 na wanawake 183.

**ALIA MATUTA BARABARANI**

Mbunge wa Viti Maalum, Bupe Mwangata (CCM), amesema matuta yaliyoko katika barabara za Rukwa yamekuwa yakiharibu viuno vya wanaume wa mkoa huo.

Bupe alitoa kauli hiyo bungeni jijini hapa jana alipochangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka ujao wa fedha (2022/23).

Alisema barabara ya kutoka Tunduma hadi mjini Sumbawanga ina matuta mengi ambayo yamesababisha viuno vya wanaume wa Mkoa wa Rukwa kutofanya kazi vizuri.

"Serikali inapata ugumu gani wa kuondoa yale matuta? Yale matuta yanatuletea matatizo yale, matatizo ni makubwa sana, hata magari yanaharibika," alilalama.

Mbunge huyo alisema barabara hiyo imekuwa ni tegemeo kwa uchumi wa taifa, huku akikatishwa kuendelea mchango wake bungeni pale mmoja wa wabunge wanaume aliposimama na kuomba kumpatia taarifa mchangiaji kuwa anachokisema ni kweli barabara hiyo imesababisha wanaume wa Mpanda waliomo ndani ya Bunge walalamikie viuno vyao kutokuwa sawa.

"Ninataka kumpa taarifa kuwa ni kweli hoja ya matuta na viuno kwa wanaume wa Mpanda wamethibitisha wanalalamika sana humu ndani ya hili jengo (bungeni)," alisema mbunge huyo na kuibua vicheko kwa wabunge.

Bupe alisema anapokea taarifa hiyo kwa mikono miwili kwa sababu amewaona wanaume wa Mkoa wa Rukwa wanavyopata shida na matuta hayo na kwamba nyumba nyingi zinavunjika na chanzo ni matuta hayo yaliyowekwa barabarani.

Alikumbusha kuwa Rais John Magufuli wakati wa uhai wake, alimwagiza waziri anayehusika na ujenzi kuondoa matuta hayo ndani ya mwezi mmoja, lakini agizo hilo halikutekelezwa.

Aliongeza kuwa hata Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambaye hakumtaja, alipofanya ziara mkoani humo hakulala usiku mzima kwa sababu ya shida ya mgongo aliyoipata kutokana na matuta hayo.

Mbunge huyo alirejea uamuzi wa kiongozi huyo wa chama kwamba alitoa maagizo ya kuondolewa kwa matuta hayo ndani ya wiki mbili, lakini agizo lake halikutekelezwa.

# LHRC yaona mabadiliko uhuru wa kujieleza nchini

**Na Sabato Kasika**

TANZANIA imeonyesha mabadiliko kidogo katika uhuru wa kujieleza huku ikitajwa kuendelea kushikilia nafasi ya 124, katika suala la uhuru wa vyombo vya habari duniani kwa mwaka 2021.

Hayo ni sehemu yale yaliyotolewa katika ripoti ya haki za binadamu ya mwaka 2021na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), iliyotolewa jijini Dar es Salaam jana.

Akitoa ripoti hiyo kwa vyombo vya habari, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema sheria na kanuni bado ni changamoto hasa zile zenye vikwazo katika ufurahiaji wa haki hiyo ikiwamo Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016.

"Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015, na Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta. (Maudhui ya Mtandaoni) Kanuni za mwaka 2020 na mwaka 2021," alisema Henga.

Alisema kituo hicho kiliweka kumbukumbu ya matukio saba ya ukamataji usio halali wa waandishi wa habari.

"Katika hali ya upatikanaji na ufikiwaji wa haki na haki jinai nchini, mwaka 2021, serikali na mahakama ziliendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa majengo ya mahakama, uteuzi wa majaji wapya, kuajiri mahakimu na matumizi ya TEHAMA ili kuimarisha upatikanaji wa haki na utekelezaji wa mapendekezo yaliyopendekezwa ikiwamo upanuzi wa programu ya mahakama zinazotembea," alisema.

Alisema pamoja na jitihada hizo za upatikanaji wa haki, utafiti wao umebaini kuwa upatikanaji wa haki unawindwa na changamoto kadhaa ikiwamo rushwa ambayo ndio ilitajwa kuwa kikwazo kikubwa zaidi na asilimia kubwa ya wananchi walioshiriki katika utafiti huo, asilimia kwa 79 ikifuatiwa na muda au urefu wa mashauri katika mahakama za sheria asilimia 48, uelewa mdogo wa sheria miongoni mwa wananchi asilimia 47, na gharama za uwakilishi wa kisheria asilimia 37.


**UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**TANZANIA ELECTRIC SUPPLY COMPANY LIMITED**

TANESCO

**Specific Procurement Notice**
**Invitation for Prequalification**

**Country: United Republic of Tanzania**
**Name of Project: Engineering, Procurement and Construction Inyonga and Loliondo Diesel Solar PV Hybrid Power Plants**
**Contract Title: For prequalification of EPC contractors for Engineering, Procurement and Construction of Solar PV-Diesel Hybrid Power Plant in Inyonga and Loliondo**
**Prequalification Reference No.: PA/001/2021-22/HQ/W/013**

Issued on: 12th April, 2022

The **Government of the United Republic of Tanzania** has received funds from Agence Française de Développement ("AFD") toward the cost of the Construction of Solar PV-Diesel Hybrid Power Plant in Inyonga and Loliondo, and it intends to apply part of the funds to payments under the contract For Engineering, Procurement and Construction of Solar PV-Diesel Hybrid Power Plant in Inyonga and Loliondo:

**The Tanzania Electric Supply Company Ltd (TANESCO) intends to prequalify Firms for prequalification of EPC contractors for Engineering, Procurement and Construction of Solar PV-Diesel Hybrid Power Plant in Inyonga and Loliondo.**

Interested eligible Applicants may obtain further information from the **Tanzania Electric Supply Company Limited (TANESCO)** during office hours from 0800 hours to 1700 hours at the address given below. A complete set of the Initial Selection Documents in English may be purchased by interested Applicants (a) on the submission of a written application to the address below and (b) upon payment of a nonrefundable fee of 100 USD (United State Dollars two hundred Only) or its equivalent in a freely convertible currency) - **transaction charges exclusive payable by Applicant**. The applicant himself or his agent shall collect the Prequalification Documents at the Employer's office from **8:30Hours to 15:30Hours** in normal working days.

The prequalification documents may also be delivered to Applicants by email in PDF format through Applicant's email address provided to the Client, upon submission of proof of payment of the application fee, **(Note: Applicants must provide reliable address to avoid any communication difficulties).**

Applicant shall transmit a copy of Bank Payment Slip and his e-mail address to the e-mails below, **(Note: Applicants must make sure that, the payment for application fee covers all Bank charges).** The e-mail addresses are: - **sec.tenderboard@tanesco.co.tz and pmuprojects@tanesco.co.tz**.

Local Interested Applicant may buy Prequalification Documents at TANESCO premises and pay locally through National Microfinance Bank (NMB) upon receipt of reference number from TANESCO.

Bank Accounts for Payment of Application Subscription Fees for Transactions from Abroad

| | Currency | Bank | Account | SWIFT Code |
|---|---|---|---|---|
| 1 | EURO | CRDB Bank | 19J1043011100 | CORUTZ |
| 2 | USD | CRDB Bank | 02J1043011100 | CORUTZ |
| 3 | USD | CITI Bank | 0100235021 | CITITZTZ |

Applications for prequalification should be submitted in clearly marked envelopes and delivered to the address below by 10.30 hours East African Time on Thursday, 13th May, 2022. Late applications shall be rejected. The address referred to above is: -

**Secretary Tender Board**
**Tanzania Electric Supply Company Limited**
**Umeme Park Building, Ground Floor, Room No. G04**
**Morogoro Road, Ubungo Area,**
**Dar Es Salaam, TANZANIA**

**Attn: Ms. Rehema O. Shabani**
**P. O. Box 9024**
**Dar es Salaam, TANZANIA**
**Tel: +255 22 221 0231, +255 22 221 0232**
**E-mail: sec.tenderboard@tanesco.co.tz; pmuprojects@tanesco.co.tz**
**Web site: www.tanesco.co.tz**

**The fee, if any, shall be to defray printing and mailing/shipping costs and shall be nominal.**

216799102

HABARI KITAIFA

# Gwajima 'aliamsha dude' bungeni

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima (CCM), ametahadharisha kuwa kama taifa halitakuwa na maono, litasababisha kila Rais anayeingia madarakani kuanza na chake.

Amesema hali hiyo ikiachwa iendelee, ipo siku Tanzania itapata kiongozi wa ajabu na kuangukia pua.

Askofu Gwajima, maarufu 'Mzee wa Kuliamsha Dude', alitoa kauli hiyo bungeni jijini hapa alipochangia makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Waziri Mkuu na taasisi zake kwa mwaka ujao wa fedha.

Alisema ipo sababu inayoifanya Tanzania ibaki ilipo kwa muda mrefu, akisisitiza kuwa inahitaji dira, ajenda, maono au mwelekeo wa taifa.

Alibainisha kuwa amefika katika nchi 143, akikumbana na mshangao mataifa ya Afrika yote yana asili ya kufanana, yana matatizo yanayofanana na yako nyuma kwa aina inayofanana.

Askofu Gwajima alisema amebaini mataifa hayo hayana maono ya muda mrefu ambayo yanalifanya taifa liongozwe katika mamlaka.

Aliutolea mfano Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), akisema kuwa wana mpango wa mwaka 2050 hadi 2117 kuhamishia makazi katika sahari ya Mars.

Pia, alisema muungano huo una mpango wa kuwa nchi ya kwanza duniani kwa kuwa na hifadhi kubwa ya chakula. Alisema hakuna nchi iliyoendelea duniani bila kuwa na mpango wa muda mrefu na kwamba kusipokuwa na mpango wa maendeleo wa muda mrefu, kasi ya Tanzania kimaendeleo haitaenda kama inavyotakiwa.

Askofu Gwajima alisema Ibara ya 63 kifungu cha 3C cha Katiba ya Tanzania, inaliruhusu Bunge kujadili na kuidhinisha mpango wowote wa muda mrefu ama mfupi unaokusudiwa kutekelezwa na kutunga sheria ya kusimamia mpango huo.

Alisema kuna hatari itakayolipata taifa siku zijazo na ndiyo maana watu wamekuwa wakisema wanahitaji Rais mwenye maono na hayo yote yanatokea kwa sababu nchi haina maono.

"Tunahitaji maono ili kila Rais anayeingia madarakani afuate maono tulioyiwekea. Ipo siku kama tutaruhusu kila anayeingia madarakani aongozwe na kichwa chake, kuna siku tutapata Rais wa ajabu, tutadondokea pua na hatutaamini macho yetu," alitahadharisha.

Alisema kuwa baada ya vita vya pili vya dunia, nchi za Ulaya zilifilisika, lakini Marekani walianzisha mpango maalumu wa kuzisaidia nchi za Ulaya Magharibi 17 ambazo zilifilisika kabisa.

Mbunge huyo alisema Marekani iliwapa Dola bilioni 13 ambazo kwa sasa ni sawa na Dola bilioni 115 na kuwataka kutengeneza mipango yao ya muda mrefu.

Alisema awamu zilizotangulia zilifanya vizuri, lakini hazikuendeleza kilichoasisiwa na kila awamu, kwamba kila kiongozi alikuja na mambo yake, hakuendelea alipoishia mtangulizi wake.

"Tumekuwa na Mwalimu (Julius) Nyerere, aliendelea kwa namna yake. Akaja (Ali Hassan) Mwinyi ameenda kwa namna yake, lakini alipoishia Mwinyi, Mheshimiwa (Benjamin) Mkapa hajaendelea pale. Alipoishia Mkapa, (Jakaya) Kikwete hajaendelea na (Dk. John) Magufuli hivyo hivyo.

"Tunakuwa na kila Rais anaingia madarakani anaanza chake na matokeo yake tukipata Rais wa ajabu, tutaangukia pua hujawahi kuona," alitahadharisha.



Diwani wa Kata ya Luhunga wilaya ya Mufindi mkoani Iringa Adam Mgovano akivuka daraja la shambani Mto Kipemba kijiji cha Lulanda kata ya Ihanu jana: **PICHA NA FRANCIS GODWIN**

# Kunyongwa hadi kufa kwa mauaji

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Dodoma, imemhukumu fundi ujenzi Menruf January Haule (42) kunyongwa hadi kufa kwa kosa la kukusudia la kuwaua kwa kutumia sululu walinzi wawili wa kituo cha kuuza mafuta cha state Oilcom kilichopo eneo la Kisasa jijini Dodoma.

Katika kesi hiyo ya Jinai Namba 47 ya mwaka 2020, Haule alifanya tukio hilo Septemba 2015 kwa kuwapiga kichwani kwa kutumia sululu Paul Nduruma na Aloyce Patsango

kwa madai walikuwa wakimnyanyasa katika shughuli zake za ujenzi.

Jaji Dk. Adam Mambi alisema siku ya tukio mshtakiwa alimaliza kazi zake na kuondoka na sululu ambayo aliificha katika shimo na ndio iliyotumika katika mauaji hayo.

Jaji alisema mshtakiwa alirudi eneo la tukio bila ya walinzi kujua na kusubiri muda wa saa sita usiku ambapo walinzi hao walikuwa wamelala ndipo alimpiga Nduruma kichwani mara mbili na baadae kumfuata Aloyce Patsango na kumpiga mara tatu kichwani.

Jaji Dk. Mambi alisema baada ya kutekeleza tukio hilo Haule alivunja kontena na kuiba mifuko ya saruji 60 aina ya twiga na kumpigia simu Mustapha Rajabu ambaye ni shahidi ili aweze kumuuzia kwa bei ya Sh. 10,000 kwa kila mfuko.

Hata hivyo Jaji Dk. Mambi alisema katika kesi za mauaji mara nyingi wanaangalia ushahidi wa mazingira kutokana na kwamba wauaji huwa wanajificha ili wasijulikane na kuongeza kuwa kitendo cha shahidi wa kwanza, watatu,wanne na watano kutoa ushahidi wao unaofanana moja kwa moja ushahidi wa mazingira unamtia hatiani mshtakiwa.

Pia mahakama iliangalia maoni ya wazee wa baraza ambapo ilijikita katika kuangalia hoja kama mshtakiwa anahusika katika mauaji hayo.

Jaji Dk. Mambi alisema baada ya ushahidi huo kukamilika mshtakiwa anahukumiwa kwa kifungu cha sheria cha 196 na 197 cha kanuni za adhabu ambapo mshtakiwa anapotenda kosa la kuuwa kwa kukusudia adhabu yake huwa ni moja kunyongwa hadi kufa.

Hata hivyo alisema mshtakiwa anaruhusiwa kukata rufaa kama hajaridhika na uamuzi wa mahakama.

## Mkenda: Elimu ya juu inaporomoka

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema elimu ya juu inaporomoka huku akishangaa kushuka kwa viwango vya kupata uprofesa.

Hali hiyo imemfanya ayatake Mabaraza ya Vyuo Vikuu nchini kuwapo na ubora kwa kutoshusha vigezo ili kupata watu wengi.

Alitoa kauli hiyo jana alipokuwa akifungua Baraza la Wafanyakazi wa wizara hiyo lililofanyika jijini hapa.

Alisema viwango vya kutoa uprofesa lazima vipandishwe badala ya kuwa na kila mtu profesa.

"Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kina university standards (vigezo vya chuo), lakini wanashangaa mbona wengine wanapata uprofesa kwa viwango tofauti na mishahara tofauti na ni serikali ile ile," alisema.

Pia, alisema kuna baadhi ya vyuo shahada za walimu wake zinatia shaka na kusisitiza lazima elimu ya vyuo vikuu iangaliwe.

"Tunataka akiwa profesa wa uhandisi awe ni profesa kweli kweli, tuone anazalisha watu kwa ajili ya SGR (reli ya kisasa) wanatusaidia kurekebisha ndege tunazonunua, lakini sio kujaribu kujenga mazingira ya kila mtu apate," alisema.

Alipendekeza elimu ya juu iwe na viwango na kuwa na uhitaji wa vyuo vingi zaidi bila kushusha viwango.

"Nasema hili ingawa wengine watakasirika elimu ya juu inaporomoka, yaani walimu wale wale, mitaala ile ile, jina tu, kutoka chuo sijui cha nini kuwa chuo kikuu, mwanzoni tulikuwa na tabia chuo kinataka kuwa chuo kikuu kishikizwe na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kilipoanza kilishikizwa na Chuo Kikuu London kusimamia ubora kwa hiyo unaanza kujijenga kuwa chuo kikuu huku unasimamiwa na chuo kikuu kingine kusimamia ubora, baadaye tukaona hatuwezi kujisimamia wenyewe kikawa Chuo Kikuu Afrika Mashariki, ambapo ilikuwa Chuo cha Dar es Salaam, Makerere na Nairobi."

"Sokoine iliangaliwa na Chuo Kikuu Dar es Salaam sasa hivi mtu anataka atoboe hapo hapo aende, mtu hataki kuatamiwa kwa sababu kuna baadhi ya vyuo hata digrii za walimu zina mashaka, kuna chuo kilikuwa kinaongozwa na Makamu Mkuu wa Chuo ambapo shahada yake inatokana na NGOs yaani zile digrii ambazo unalipa kiasi fulani unapata, lakini ukiajiriwa tutakuuliza digrii yako ni ipi? Ukiajiriwa na serikali tunataka kujua PhD yako ulipata wapi," alisema.

Kadhalika alisema kama watashindwa kusimamia viwango vya elimu ya juu mageuzi yatazungumzwa hadi mwisho wa dunia.

Alihimiza kuongeza ubora wa elimu ili vijana wanaohitimu waajirike na kuajiri.

"Katibu Mkuu wetu hapa alipoingia wizarani alisema utengenezaji wa magari ya wizara ufanywe na VETA kwa kuwa wanafundisha utengenezaji magari, wakasema aah! Tunaomba ukaombe kibali TEMESA, yaani unapewa kazi unakataa, tunachukua vijana tunasema tunawafundisha ufundi magari hivi kweli tunawafundisha ufundi magari au tunadanganya wazazi," alihoji.

Prof. Mkenda alisema atafanya uamuzi wa kuimarisha ubora wa elimu na sio kubembelezana na kwamba elimu inayotakiwa kutolewa ni ya kumuwezesha kijana kujiajiri na kuajiriwa.

Hata hivyo, alisema elimu ni uwekezaji wa vizazi na vizazi na kwamba uwekezaji ukifanywa vizuri itakuwa ni kuwekeza katika maendeleo ya nchi.

Akizungumzia kuhusu sera, Prof.Mkenda alisema sera ya elimu ya mwaka 2014 inataka mtoto asome kwa miaka 10 elimu ya lazima suala hilo halijafutwa na kwamba sera hiyo ipitiwe na wakubaliane au wabadilishe sera.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Prof. Eliamani Sedoyeka, alisema baraza hilo linajukumu la kuishauri wizara na kuhakikisha utekelezaji wa majukumu yanafanyika kwa weledi.

TANGAZO


NMB
Karibu yako
TELEZA
KIDIJITALI
NMB MSHIKO FASTA
Mkopo
Papo Hapo
Bila
Dhamana
NMB mkononi
*150*66#
App Store
Google Play
Akaunti | Miamala | Mikopo | Malipo
Papo Hapo! #NafuuRahisiSalama
Vigezo na Masharti kuzingatiwa
www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunataka uwajibikaji watumishi wa umma

**JUZI,** Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Abdulrahman Kinana, aliwataka viongozi wenye nafasi mbalimbali kuacha kujikweza na kutaka utukufu badala yake wawe watumishi wa wananchi ambao wana wajibu wa kuwatumikia.

Alisema miaka ya karibuni kumekuwa na tabia ya watu kujikweza kutaka utukufu kutoka kwa watu wanaowatumikia, huku wakisahau kuwa kazi nzuri inayofanywa na muhusika itamfikisha kwenye utukufu kuliko kulazimisha kutukuzwa.

Aidha, kwa kuanza ameahidi kuwa mfano wa kuwa mtumishi wa watu na siyo kutaka kutukuzwa, huku akiahidi kuwafikia wananchi kwa kufanya ziara.

Tunaunga mkono kauli ya Kinana kuwa kuna wakati dhana ya mtumishi wa umma ilipotea na kuwa na watu wenye kutaka kuabudiwa, kutukuzwa kunyenyekewa kupita kiasi wakati wako kwenye ofisi za umma wanawajibika kuwatumikia walipa kodi.

Wapo watumishi waliotumia vibaya ofisi za umma kujitajirisha na watu wao wa karibu, wengine wakiota majipu kwenye makwapa (kiburi, kujikweza) kutokana na kujikweza mbele ya umma kwa sababu ya nguvu ya fedha na nafasi walizonazo.

Wengi wanasahau cheo ni dhamana na unapoaminiwa unatakiwa kulipa imani, badala yake wananchi ambao ndiyo mabosi wao wanawadharau , huku wakisigina kanuni na sheria zilizopo.

Kanuni za utendaji katika utumishi wa umma za mwaka 2005 zinasema ili utumishi wa umma uwe wenye ufanisi na wa kuheshimika, watumishi wanapaswa kuzifuata kanuni za maadili ya utumishi pamoja na kuwa na tabia na mwenendo unaozingatia kutoa huduma bora, utii wa serikali, bidii ya kazi, kutoa huduma bila upendeleo, kufanya kazi kwa uadilifu, kuwajibika kwa umma , kuheshimu sheria na matumizi sahihi ya taarifa.

Kanuni hiyo inasema huduma bora ni kuweka malengo halisi ya kazi, ili kuwawezesha kufikia kiwango cha juu kabisa katika utendaji wao wa kazi. Pia, inawataka kuwa wabunifu, wavumbuzi na siku zote kujibidiisha kuongeza viwango vya utendaji kwa kujiongezea maarifa na ujuzi.

Aidha, wanatakiwa kutumia misingi ya haki, badala ya upendeleo katika utoaji wa huduma, kuepuka kufanya vitendo viovu au kutamka maneno yanayolenga kuwaaibisha watumishi wa ngazi moja, za chini au wa vyeo vya juu.

Pia, wanatakiwa kuepuka matumizi ya lugha mbaya, matusi, utani na hasira katika utendaji wa kazi, kupeuka mwenendo mbaya ambao utaathiri ufanisi katika utendaji kazi, kufika sehemu ya kazi kwa muda uliopangwa na kuzingatia muda rasmi wa kufanyakazi.

Haya ni machache kati ya mengi ambayo yakifuatwa yatamtambulisha mtumishi sahihi anayelipwa kwa kodi za watanzania, lakini baadhi wametaka kuwa miunguwatu kwa sababu ya vyeo hivyo.


Wapo walioonekana kutumia nafasi zao kuwanyanyasa wananchi wazi kwa kutumia maneno yao, kiasi cha wao kuwa kama waliowaajiri wananchi na siyo wameajiriwa, huku wengine wakijipatia utajiri bila hofu yoyote.

Katika baadhi ya ofisi za umma watumishi hawatimizi wajibu wao ipasavyo huku wakisema serikalini hakuna haja ya kukimbizana na kazi kama sekta binafsi, na hilo hudhihirika zaidi Rais, Makamu wa Rais au Waziri Mkuu wanapofanya ziara kwenye eneo la wananchi huibua kero ambazo zinastahili kutatuliwa na watumishi wa ngazi za chini.

Ni lazima watumishi wawe karibu na wananchi katika kutatua kero zao, kama alivyoona Kinana nasi tumeona kuna tatizo kubwa kwa watumishi wengi ni lazima kufuatilia kwa karibu ili kurejesha nidhamu na uwajibikaji.

Ofisi za umma isiwe ni sehemu ya kutengeneza miungu watu ambao wanatumia kodi za watanzania, bali wawepo kwa ajili ya kutoa huduma bora kwa kuwa ni wajibu wao kuwajibika kwa mujibu wa maadili ili kupunguza mzigo na lawama kwa viongozi wa ngazi za juu.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Maisha mapya mtaa Makoroboi ya Mwanza toka zama 'vurugu mechi'

Anthony Gervas

**KATIKATI** ya jiji la Mwanza kuna mtaa maarufu unaoitwa Makoroboi. Ni jina linalotokana na wajasiriamali wa wakati huo waliokuwa wakitengeneza koroboi au vibatari na kuuza bei ya jumla na rejareja. Hiyo ilichangiwa na maeneo mengi kukosa nishati ya umeme mjini na vijijini.

Zama hizo ukitaka kupata taa aina ya koroboi au kibatari, uwe unatoka kijijini au mjini, Mwanza, ni lazima utakwenda kununua katika mtaa huo, ndiko zilikuwa zinatengenezwa kwa wingi na kuuzwa kwa bei tofauti, kulingana na ukubwa wake.

Leo hii, ni kama simulizi kuamini kwamba imebaki historia kuwa machinga waliokuwa wakipambana kuondoka katika eneo hilo baada ya serikali kuagiza machinga kuondolewa katikati ya jiji na kuhakikisha wanapelekwa kwenye maeneo yao waliyotengewa.

Katika miaka yote kihistoria katika mtaa huo wa Makoroboi walikuwa wakipambana na vyombo vya dola, wanapoondolewa,vurugu zilikuwa zikitawala kurushiwa mawe mgambo wa jiji hata askari wengineo na kulazimika kutumika nguvu kubwa ya kuwapiga mabomu ya machozi na magari ya washawasha, ili kuwatawanya waweze kuondoka kwenda kwenye maeneo yao rasmi waliyopewa.

Ni msuguano uliochangia watu wengi kupoteza maisha au kujeruhiwa na kupata ulemavu, wachache waliondoka, lakini baada ya muda mfupi, wanajaa tena eneo hilo. Wapo wanaosifika walikuwa nyuma yao bila ya kujali athari zake.

**Ni msuguano uliochangia watu wengi kupoteza maisha au kujeruhiwa na kupata ulemavu, wachache waliondoka, lakini baada ya muda mfupi, wanajaa tena eneo hilo. Wapo wanaosifika walikuwa nyuma yao bila ya kujali athari zake.**

Mtaa huo, pia ni njia maarufu wanayopita watu mbalimbali wanaotoka nje ya jiji hilo katika mikoa mbalimbali, wale wanaokwenda mjini kila siku hawawezi kumaliza siku nyingi bila ya kupita mtaa huo, ambao ulikuwa umesheheni maduka ya nguo na bidhaa mbalimbali wakiwemo mama lishe.

Machinga hao walikuwa ni vigumu kuwaondoa kutokana na mambo ya kisiasa, lakini serikali imeweza kufanikiwa kupaweka tofauti katika tafsiri mpya.

Wafanyabiashara hao wadogo, walikuwa wamejenga vibanda vyenye gharama kubwa na kuweka mbele ya maduka mengine ya wafanyabiashara wakubwa, kila aina ya bidhaa zilikuwa zikipatikana.

Machinga wengine walitumiwa na wafanyabiashara wenye maduka makubwa kufanya biashara hizo, lengo ni kukwepa kodi za serikali wanazotakiwa kulipa kihalali, hapo ndipo wengi wao wataumbuka na kuonekana biashara zao wanavyoziendesha.

Mimi binafsi naishukuru serikali kuwapeleka katika maeneo yao waliyotengewa, wengi walikuwa wakifanya biashara zao katika maeneo hatarishi, walijenga vibanda juu ya mifereji, mitaro na kusababisha kuziba,kutoa harufu mbaya pamoja na uchafuzi wa mazingira.

Ulikuwa mchango mkubwa kwa jiji la Mwanza hata likashuhudiwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira, leo hii linabadilika kurejea katika usafi ukawa changamoto yenye sura yake. Hivi sasa, jiji limehamia sura mpya hata wananchi wameona kumbe serikali inawapeleka kwenye maeneo sahihi.

Kazi iliyobaki ni watendaji wa serikali kusimamia maeneo ya machinga walikopelekwa, kuhakikisha miundombinu muhimu ipo katika masoko hayo, mifereji, mitaro, barabara, umeme, maji na usafi wa mazingira, ili kuepuka wakati wa mvua magonjwa ya milipuko kama vile kipindupindu yasiibuke.

Tukumbuke, Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye hotuba yake wakati akiingia madarakani kuwa anaona mbali na akawataka watendaji wa serikali kuchapa kazi kwa bidii na maarifa kuwahudumia wananchi.

# Dar, Tanga zazorota anwani za makazi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, amesema operesheni ya uwekaji wa anwani za makazi kwenye mikoa ya Tanzania bara imefikia asilimia 68 huku akiitaja mikoa ya Dar es Salaam na Tanga kutofanya vizuri.

Kutokana na hali hiyo, ameanza ziara nchi nzima kwa ajili ya kuhamasisha, kufuatilia mwenendo wa operesheni hiyo ili kuona utekelezaji unavyokwenda na kuongeza nguvu kwenye maeneo yanayosuasua.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Uwanja wa Ndege wa Dodoma, kabla ya kuanza ziara hiyo kwenye mikoa ya Tanga, Kilimanjaro na Arusha, Waziri Nape, alisema katika baadhi ya maeneo wanalazimika kuongeza nguvu kupeleka wataalamu zaidi.

"Tathmini yetu inaonesha tumefikia asilimia 68.69, lakini bado kuna baadhi ya maeneo changamoto kuna mikoa ambayo bado haifanyi vizuri sana ikiwamo Dar es Salaam na Tanga, hii kazi tunatakiwa kukabidhi ifikapo Mei 22, mwaka huu, muda umeisha, kwa muda uliobaki tumekubaliana tuongeze nguvu katika kuongeza hamasa na ukaguzi," alisema.

Vile vile, alisema tathmini waliyoifanya imeonyesha kuwa kuna mikoa inafanya vizuri ikiwamo Mkoa wa Lindi

"Nakwenda 'site' kuona zipo sababu kadhaa, tumefanya vikao vya kuulizana kwanini wengine wanafanya vizuri na wengine wanafanya vibaya, sasa majibu waliyoyatoa ndiyo yametufanya tuone sababu ya kwenda site kwenda kuona uhalisia ulivyo," alisema.

Alisema mikoa iliyofanya vizuri pia itatembelewa ili kujua mbinu walizotumia hadi kufanikiwa kufanya vizuri.

"Kwa mfano Mkoa wa Pwani tofauti ya wilaya ni kubwa sana sisi wizarani tumetengeneza mfumo ambao tunaona kila siku maendeleo yakoje? Unakuta wilaya moja imefikia asilimia 80, nyingine imefikia asilimia 20 lazima muende mkasukume sukume."

"Tumeamua kwenda site wenyewe ndani ya muda mfupi katika operesheni hii tuone namna ya kurekebisha tunawasaidiaje kwanza wale ambao hawafanyi vizuri tunaongeza wataalam kule kwenye maeneo yao kuwasaidia kuwashauri na sisi wenyewe kuendelea kuwafuatilia na ziara hii ni muendelezo wa huo msaada," alisema.

Alitoa wito kwa Watanzania kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan, kufanikisha operesheni hiyo aliyoizindua na kuipa jina la anwani ya makazi.

Katika ziara hiyo, Waziri Nape ameambatana na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Jim Yonazi, na baadhi ya wataalamu kwa kutumia usafiri wa helkopta ili kuifikia mikoa zaidi ya mitatu kwa siku.

## Baba akataa kumuozesha binti ili asome kwanza

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

NGASA Selelim, mkazi wa Kijiji cha Welezo wilayani Shinyanga, amekataa kumuozesha binti yake mwenye umri wa miaka 18 (jina tunalihifadhi), kwa maelezo kuwa haoni faida ya kuozesha badala yake amemtaka asome na kutimiza ndoto zake.

Msichana huyo amehitimu elimu ya kidato cha nne mwaka jana na hakupata matokeo mazuri, lakini akiwa bado yupo shuleni alijaza fomu ya kujiunga na Chuo cha Elimu ya Ufundi Tarime, lakini kutokana na ugumu wa maisha nyumbani kwao ameshindwa kujiunga na chuo hicho.

Seleli akizungumza na Nipashe ilipotembelewa katika kijiji hicho juzi, alisema anatamani binti yake huyo apate wafadhili ambao watamsaidia kumlipia ada ili akasome kwenye chuo hicho na kutimiza ndoto zake ili aisaidie familia yake ambayo inaishi maisha duni.

"(Anamtaja jina) ni mtoto wangu wa nne na katika familia yangu nina watoto watano, watatu wa kiume na wawili wa kike, dada yake, Veronica Ngassa yeye aliolewa alipomaliza darasa la saba na maisha yake siyo mazuri, ndiyo maana kwa huyu binti yangu nimegoma kumuozesha, nataka asome sababu sioni faida ya kumuozesha," alisema Seleli.

"Nimekuwa nikishawishiwa sana kuwa nimuozeshe binti yangu, kwa sababu huku vijijini kawaida mtoto akimaliza shule tayari watu wanakuja kumtolea mahari ya ng'ombe, lakini baada ya kuchekecha akili nimejifunza kutoka kwa dada yake nikaona haina haja ya kumuozesha, nataka asome japo sina uwezo," aliongeza.

Binti huyo aliwaomba wadau kumsaidia ada ili akasome kutimiza ndoto zake, kwa sababu wazazi wake hawana uwezo wa kumsomesha, na yeye hataki kuolewa akiwa bado mdogo na kuishia kuteseka, kutokana na kuwaona wenzake namna wanavyoteseka na maisha.

Aidha, alisema kwa mujibu wa fomu ambayo wamepewa ya kujiunga na chuo hicho, anatakiwa kulipia Sh. milioni 1.4 kwa mwaka, hivyo kuwaomba wadau wamsaidie asome.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu LHRC, Anna Henga (katikati) na wadau wengine wa haki za binadamu wakizindua ripoti ya haki za binadamu ya kituo hicho ya mwaka 2021 jijini Dar es Salaam jana. **PICHA : SABATO KASIKA**

## Kikao cha kuimarisha mpaka wa Tanzania, Kenya chaanza

**Na Munir Shemweta,** TARIME

Kikao cha kamati ya pamoja ya wataalamu wa mipaka kati ya Tanzania na Kenya kilianza jana wilayani Tarime mkoa wa Mara.

Kikao hicho kinatarajiwa kumalizika Ijumaa na kutoa muongozo juu ya namna bora ya kutekeleza kazi iliyobaki.

Akizungumza katika ufunguzi wa kikao hicho kwa niaba ya mkuu wa mkoa, Mkuu wa wilaya ya Tarime, Kanali Michael Mangwela, alisema uimarishaji mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya ulenge kuimarisha mahusiano ya nchi hizo pamoja na kujadili vikwazo vya maeneo ya mipakani.

"Pamoja na kuimarishwa mipaka kati ya Tanzania na Kenya, lakini bado kuna maeneo ambayo baadhi ya wananchi kutoka kila upande wanaingia na kuendesha shughuli zao, hivyo mjadili changamoto hizi kwa kina na kuja na maamuzi yatakayoleta tija," alisema Kanali Mangwela.

Timu ya wataalamu wa Tanzania na Kenya imefanikiwa kukamilisha uimarishaji mpaka wa kimataifa wa awamu ya kwanza na kuanza awamu ya pili iliyosimama kutokana na changamoto mbalimbali.

Mwakilishi kutoka Wizara ya Mambo ya Nje ya Kenya, Balozi Joseph Vungo, aliwataka wataalamu wanaoshiriki kikao hicho kuhakikisha wanajadili na kuzitolea maamuzi changamoto kwa amani hasa wakizingatia Tanzania na Kenya zimekuwa na mahusiano mazuri.

Kwa mujibu wa Balozi Vungo, maamuzi yoyote yatakayoamuliwa katika kikao hicho yalenge kuleta tija na kudumisha mahusiano mazuri yaliyopo.

Zoezi la uimarishaji mpaka wa kimataifa kati ya Tanzania na Kenya awamu ya kwanza limeanzia hifadhi ya Serengeti / Masai Mara kipande cha Kilomita 60 hadi eneo la Ziwa Natron kilomita 23 na awamu ya pili inaanzia Ziwa Natron hadi Namanga eneo la Kilomita 110.

# PM azipa somo taasisi za fedha

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amezitaka taasisi za fedha kubuni mikakati na mbinu zitakazowezesha watanzania wengi kupata huduma rasmi za kibenki kwa gharama nafuu ili kujiongezea kipato na kujikwamua na umasikini.

Alitoa wito huo jana katika hafla ya huduma ya Teleza Kidijitali inayotolewa na Benki ya NMB, iliyofanyika jijini Dodoma, huku akizishauri taasisi nyingine za kifedha ziige utoaji wa huduma kwa njia hiyo.

Alisema taasisi hizo hazinabudi kuiunga mkono Serikali kwa kubuni mikakati mbalimbali ya kuhamasisha matumizi ya teknolojia katika kukuza uchumi sambamba na kubuni masuluhisho rahisi kwa watumiaji wa kawaida.

"Hongereni NMB kwa ubunifu huu ambao utavutia makundi yote ya kijamii, huduma hii itawezesha wateja wenu kupata huduma ya mikopo kiganjani."

Waziri Mkuu alisema: "Yaani mtu anataka mkopo wa Sh 300000, au 500000, haendi kwenye tawi lolote la benki, haonani na mtumishi yeyote wa benki, atabaki kwenye simu yake, anaomba mkopo na anaupata, hayo ni mageuzi makubwa sana katika sekta ya kibenki."

Alisema NMB kwa huduma hizo inakwenda kuchocchea maendeleo kwani wananchi wengi wataweza kupata mitaji ya mkopo wa riba nafuu, hivyo kuepukana na wajanja wanaotoa mikopo kwa riba kubwa.

NMB ilizindua huduma kubwa tatu kupitia kampeni yake ya Teleza Kidijitali, inayomwezesha mteja kupata mkopo kupitia simu ya mkononi bila kufika kwenye ofisi na bila dhamana.

Hafla hiyo pia ilishuhudiwa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Prof. Florens Luoga.

Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema huduma hizo zitaleta mapinduzi makubwa katika sekta ya kibenki nchini.

Aliitaja huduma ya kwanza ya ni mikopo kwa njia ya kidijitali ambayo NMB wameita huduma ya MshikoFasta.

"Huduma hii itapatikana kupitia NMB mkononi kwa simu za aina zote, simu janja (kwa App) ama kwa kutumia simu za kawaida (kwa kutumia USSD).

Mteja wa Benki ya NMB, kwa kutumia huduma hii ataweza kukopa mpaka shilingi 500,000 ndani ya muda mfupi, kupitia simu yake ya mkononi,"

"Haya ni mapinduzi makubwa kwenye sekta ya kibenki Tanzania na inaendelea tu kuthibitisha dhamira yetu ya kuendelea kuwa kinara katika mapinduzi ya huduma bora za kibenki na za kibunifu hapa nchini," alisema.

Alisema imezoeleka kuwa sehemu nyingi benki hutoa huduma zinazofanana na hii, kupitia mitandao ya simu, lakini kwa ubunifu waliokuja nao, wateja wa NMB watakopeshwa moja kwa moja na Benki na mikopo hii inaweza kurejeshwa ndani ya siku 1, siku 7, 14, 21 au siku 28.

Zaipuna alisema lengo ni kuhakikisha urahisi na uharaka wa kupata mikopo husuani kwa makundi ya wajasiriamali wadogo na wa kati, kama mama lishe, bodaboda, machinga ambao wengi hawako kwenye mfumo rasmi kuwawezesha kupata mikopo kwa urahisi, kwa sababu ya aina za biashara zao, au kwa kukosa dhamana kwa ajili ya mikopo.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa NMB, Dk. Edwin Mhede, alisema lengo ni kuboresha na kurahisisha huduma zao na kuzifanya kuwa za kidigitali zaidi huku wakienda sambamba na maendeleo ya kiteknolojia ulimwenguni na utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano wa NMB (2020-2025).

Gavana wa BoT, Prof. Luoga, aliipongeza NMB kwa kwenda na kasi ya maendeleo ya kidijitali na hasa kutumia vijana wao wa ndani kuanzisha huduma hizo.




Wafanyakazi wa Taasisi ya Wazalendo Tanzania (TPO) wakiwa wameshika mabango kwenye mapokezi ya Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi CCM Tanzania Bara ,Abdulrahman Kinana alipowasili ukumbi wa Diamond Jubilee kwa ajili ya wana CCM Mkoa wa Dar es Salaam juzi, kumpokea rasmi na kumpongeza mara baada ya kuchaguliwa. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Miradi UVIKO-19 Ruvuma yamtua mama ndoo kichwani

**Na Mwandishi Wetu,** RUVUMA

UTEKELEZAJI wa Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Uviko-19, kupitia sekta ya maji vijijini mkoani Ruvuma, umefikia asilimia 52, ikitajwa ni hatua ya kumkomboa mama na kumtua ndoo kichwani.

Mkoa wa Ruvuma unatekeleza miradi saba ya maji ya Sh. bilioni 4.8 ikiwa ni sehemu ya mkopo usio na riba wa Sh. trilioni 1.3 kwa serikali kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Miradi hiyo inatekelezwa katika majimbo ya Nyasa, Mbinga Mjini, Mbinga Vijijini, Songea DC, Madaba, Namtumbo, Tunduru Kusini na Kaskazini.

Akizungumza na waandishi wa habari ambao wametembelea miradi ya maji inayotokana na fedha za Uviko-19 katika Wilaya ya Nyasa, Mbinga na Tunduru, Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingiria Vijijini (RUWASA) mkoani Ruvuma, Mhandisi Rebman Ganshonga, alisema miradi hiyo imemuondolea mama adha ya kufuata maji umbali mrefu.

Ganshonga alisema miradi hiyo pamoja na kuwafanya wananchi kuchota maji bombani pia itachochea shughuli za maendeleo, kijamii na ukuaji wa uchumi.

"Miradi hii ambayo inatekelezwa kupitia fedha za Uviko-19 hadi sasa ujenzi umefikia asilimia 52 na matarajio yetu ni miradi hii saba kukamilika Mei 15, mwaka huu," alisema.

"Kukamilika kwa miradi hii kutawezesha wananchi kujikita na shughuli za uzalishaji, hivyo uchumi kukua."

Alisema wananchi ambao vijiji vyao vimefanikiwa kupata miradi hiyo wamepokea kwa mikono miwili hali ambayo inarahisisha utekelezaji, huku akimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan na serikali kwa kuwapatia fedha hizo.

Ganshonga alisema RUWASA imejipanga kuhakikisha miradi yote ambayo inatokana na fedha za Uviko-19, inakamilika kwa wakati na kwamba hawatavumilia mkandarasi ambaye atazembea.

# Waomba utaratibu maalum kuwapokea wanafunzi wa nje

**Na Mwandishi Wetu**

WATAALAM na wadau wa elimu ya juu wamewaomba viongozi wa serikali kuanzisha utaratibu maalum utakaoviruhusu vyuo vikuu nchini kuwapokea wanafunzi kutoka vyuo vya nje kusoma kozi ya shahada Tanzania.

Musa Rajab, mtaalam wa elimu alisema kuwa kwa sasa ni wanafunzi wenye alama za ufaulu sawa na elimu ya sekondari ya juu (kidato cha sita) tu ndio wanaoruhusiwa kusoma kozi ya shahada nchini, kwa mujibu wa aya ya 3.1.3 na 3.1.7 za Kiongozi cha Viwango na Mwongozo (Toleo la Tatu) cha Tume ya Vyuo Vikuu (TCU).

Alisema kigezo cha ulinganifu kilichowekwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) kuwa ni kikwazo kwa wanafunzi kutoka nchi za nje , kama vile Kenya, Sudani Kusini, Nigeria, India, Ghana na nchi nyingine nyingi duniani zinazotumia mifumo tofauti ya elimu ya sekondari.

"Wanafunzi hawa wanahitaji kozi maalumu (kozi daraja) ya kuwafanya wawe na elimu linganifu na elimu ya sekondari ya juu (Kidato cha Sita) ili waweze kupokelewa kwenye vyuo vikuu vya hapa nchini," alisema Musa Rajab, bingwa wa masuala ya elimu, hivi karibuni.

Mdau huyo alisema kuwa kwa sasa ni Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT), ndicho kilichoruhusiwa kutoa kozi ya msingi kwa wanafunzi wa Tanzania wanaotaka kujiunga na elimu ya chuo kikuu, lakini walikosa alama chache tu kuwa na sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu moja kwa moja.

Naye Mulusali Komba alisema kuwa mabingwa na wadau wa elimu hawaridhishwi na utaratibu unaoruhusu OUT pekee kutoa kozi ya msingi, huku wakizisihi taasisi za serikali kufanya marekebisho ya kimkakati ya Kiongozi cha Viwango na Mwongozo wa TCU na kuweka kipengele kitakachoruhusu vyuo vikuu nchini kutoa kozi ya msingi kwa ajili ya wanafunzi kutoka nchi za nje ambao wamesoma kwenye mfumo tofauti na Tanzania.

"Hali hii imechangia kuongeza fedha za kigeni nchini Uganda na kupanua wigo wa elimu ya juu nchini humo, nchi nyingi duniani zina utaratibu tofauti tofauti unaoruhusu wanafunzi kutoka nchi za nje kujiunga na kozi ya shahada, ingawa wanafunzi hao walihitimu masomo kutoka katika mifumo tofauti ya elimu," alisema Mulusali Komba.

Mtaalam mwingine, Andrew Moses, amesema katika mazingira ya ushindani mkubwa wa elimu ya juu Tanzania na duniani kote, TCU haipaswi kubaki na jukumu la kusimamia tu, bali kutengeneza mazingira ya kuvisaidia vyuo vya Tanzania kupata wanafunzi kutoka nje na kutoa elimu yenye viwango na ubora ili kukabiliana na ushindani wa kimataifa.

Mtaalaam mwingine, Andrew Moses, alisema katika mazingira ya ushindani mkubwa wa elimu ya juu Tanzania na duniani kote, TCU haipaswi kubaki na jukumu la kusimamia tu, bali kutengeneza mazingira ya kuvisaidia vyuo vya Tanzania kupata wanafunzi kutoka nje na kutoa elimu yenye viwango na ubora ili kukabiliana na ushindani wa kimataifa.

"Mbali na hilo, majukumu ya TCU (kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu-Universities Act Cap. 346, Kifungu cha 5(1)) yako katika maeneo matatu: kusaidia, kushauri na kusimamia. Kwa mantiki hiyo, TCU wanapaswa kuwa wabunifu, kuchukua mawazo yenye tija kutoka kwa wadau kutoka sekta binafisi na umma, na kutengeneza mazingira yatayaboresha uendeshaji na utoaji wa huduma ya elimu ya juu katika vyuo vikuu kwa faida ya nchi ya Tanzania," alisema.

Hata hivyo, akitoa ufafanuzi, Katibu Mtendaji wa TCU, Prof. Charles Kihampa, alisema taratibu na kanuni za kusahili wanafunzi kutoka nje ya nchi zipo na zimewekwa na vyuo vyenyewe kupitia kwa Kamati ya Makamu Wakuu wa Vyuo Vikuu na Vishiriki.

Alisema kama kuna wazo kwamba vyuo viruhusiwe kuendesha kozi maalum za msingi kwa wanafunzi kutoka nje ya nchi, suala hilo linapaswa kupelekwa kwenye kamati husika kujadili na kisha kuleta mapendekezo kwa TCU.

"Kuhusu hoja kwamba wanafunzi wa kigeni ni wachache katika vyuo vyetu, nadhani hilo ni suala la vyuo vyenyewe. TCU kazi yetu ni usimamizi tu...ni jukumu la vyuo husika kutangaza vyuo vyao kwa nguvu ili kuvutia wanafunzi wengi sana kutoka nje ya nchi," alisema Prof. Kihampa.

HABARI KITAIFA

## Fikra mgando kikwazo maendeleo ya vijana

**Na Francis Godwin,** IRINGA

IMEELEZWA kuwa tatizo kubwa la baadhi ya vijana katika familia zenye mazingira magumu kutojikita kuanzisha miradi ya kiuchumi ni kutokana na kujinyanyapaa wenyewe na kuwa na fikra mgando za kukata tamaa kwamba hawawezi kufanikiwa kiuchumi hata kama wakiwezeshwa .

Akizungumza katika kijiji cha Igoda Kata ya Luhunga Wilaya ya Mufindi mkoani Iringa baada ya mafunzo ya mtazamo na miradi ya kilimo na ufugaji yanayotolewa na taasisi isiyo ya kiserikali ya R - LABS Tanzania kwa vijana wa mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), Meneja msaidizi wa mradi huo, Danford Mkumba, alisema maisha ya vijana wengi ni kutawaliwa na fikra mgando, hivyo ni vigumu kufanikiwa.

Mkumba alisema vijana wanayo fursa kubwa sana ya kufanikiwa katika maisha kutokana na jitihada kubwa zinazofanywa na mradi huo wa YAM pamoja na serikali kupitia halmashauri zote nchini ambazo zimekuwa zikitenga fedha kwa ajili ya mikopo isiyo na riba kwa kundi hilo, wanawake na watu wenye ulemavu.

Alisema katika mafunzo hayo ambayo yamelenga kuwafundisha maisha bila fikra mgando yatasaidia sana vijana hao kujitambua na kuondokana na fikra hizo na kujikita katika fikra ambayo itawawezesha kusonga mbele kimaisha kwa kuwa na miradi ya kiuchumi kupitia rasilimali zinazowazunguka.

Mkumba alisema baadhi ya vijana wanaamini kuwa wakitoka katika familia duni kwao ni vigumu kufanikiwa katika maisha, ila kwa mafunzo hayo wataweza kujitoa katika fikra mgando na kwenda na fikra sahihi.

Washiriki wa mafunzo hayo Diana Yohana, Saraphina Tengelakwi na Andason Mpende wakielezea faida ya mafunzo hayo walisema wana matumaini makubwa ya kuyatumia kubadili maisha yao kwa kwenda kubuni na kuendesha miradi yao ya kiuchumi .

Diana alisema jamii inayomzunguka imekuwa ikitoa upendeleo mkubwa kwake na shida ya kutokuwa na mradi wa kufanya ni kutokana na kupata mimba za utotoni, hali iliyopelekea kukwamisha ndoto yake ya kusonga mbele kimaisha hasa katika masomo .

Hivyo alisema kwa mafunzo hayo ya kuondokana na fikra mbovu, anaamini kuwa atakwenda kuwa mfano mwema kwa kuanzisha mradi wake ama kutimiza ndoto yake ya kurudi shule kwenda kusomea ualimu ili kuja kufundisha wenzake .

# Aga Khan kutoa matibabu ya kisasa ya saratani

**Na Romana Mallya**

HOSPITALI ya Aga Khan imeweka jiwe la msingi la kituo chake cha kisasa cha matibabu ya saratani kitakachojengwa kwa thamani ya Sh. bilioni 13.8, ambacho kitatumika kama kitovu muhimu cha Mradi Mtambuka na wa Kivumbuzi wa Saratani Tanzania (TCCP).

Akizindua mradi huo juzi, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema saratani ni ugonjwa unaoathiri watu wenye umri na jinsia zote, watoto, watu wazima, wanaume kwa wanawake.

Mradi huu wa miaka minne ambao ulizinduliwa na Huduma za Afya AgaKhan (AKHS) Januari 2022, malengo yake ya mbeleni ni kupunguza maradhi na vifo vya saratani katika mikoa ya Dar es Salaam na Mwanza na unatekelezwa chini ya ufadhili wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), pamoja na Taasisi ya Kimataifa ya Maendeleo ya Aga Khan (AKF) kwa thamani ya Sh. bilioni 38 (Euro milioni 13.3).

TCCP ni mradi wa kwanza wa aina hii unaolenga kukabiliana na athari za magonjwa yasiyo ya kuambukiza Tanzania.

Unategemewa kuwanufaisha moja kwa moja takribani watu milioni 1.7 na utashirikiana na timu za usimamizi wa afya za kanda, pamoja na timu za usimamizi wa afya za halmashauri kuunga mkono uanzishwaji wa huduma za msingi za matibabu ya saratani katika vituo 100 vya awali vya afya katika mikoa lengwa.

Waziri Ummy alisema ugonjwa huo umekuwa ukikatisha maisha ya watu na kusababisha hasara kubwa kwa taifa kwa sababu unapunguza nguvu kazi na unazorotesha maendeleo ya mtu mmoja mmoja na ya taifa.

Alisema licha ya kuzinduliwa katika kipindi cha UVIKO-19, mradi wa TCCP umefanikiwa kutekeleza kikamilifu shughuli kadhaa zilizopangwa, umetoa mafunzo ya uchunguzi wa saratani ya shingo ya kizazi na matiti kwa watoa huduma za afya zaidi ya 330 na umetoa mafunzo mengine muhimu ya matibabu ya saratani.

Alisema mradi huo pia umenunua na kufunga vifaa vyenye thamani ya Sh.bilioni moja katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road na Kituo cha Afya cha Bugando, ikiwamo mashine ya kuchunguza matiti (Mammography), ambayo ilizinduliwa mwezi uliopita.

Mwenyekiti wa Kamati Kuu ya Huduma za Afya Aga Khan, Princess Zahra AgaKhan, alisema lengo la mradi huo ni kuboresha huduma na vituo mtambuka vya matibabu ya saratani nchini.

"Takwimu za Shirika la Utafiti wa Saratani la Umoja wa Mataifa zinaonyesha kwamba Tanzania inapata wagonjwa 42,000 wa saratani kila mwaka, pamoja na kuwa na kiwango cha juu cha vifo 28,000 kwa mwaka. Takribani asilimia 75 ya wagonjwa hao wanagundulika katika hatua ya mwishoni. Hii ni changamoto kubwa ambayo inaathiri uwezekano wa kupona, alisema.

Meneja Mradi Mtambuka wa Saratani Tanzania, Dk. Harrison Chuwa, alisema kama ilivyo kwa nchi nyingi za kipato cha chini na cha kati, Tanzania inasumbuliwa na ongezeko la idadi ya wagonjwa wa saratani sehemu mbalimbali nchini, na rasilimali chache za kutibu.

Alisema kwa kutumia mkakati wa hatua nne, mradi wa TCCP unalenga kuboresha na kupanua miundombinu ya mfumo wa sasa wa afya ya saratani; kujenga uwezo wa wafanyakazi wa taasisi husika; kuimarisha uelewa na ushiriki wa jumuiya kwa saratani; na kuandaa ajenda ya pamoja ya utafiti na ubia miongoni mwa washiriki wa mradi huo. Mkurugenzi wa Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD) nchini,

Stephanie Mouen, alisema anaamini kwamba mradi huo wa TCCP baada ya Kituo cha Tiba ya Mionzi kumalizika na vifaa vyote kufungwa, utafikia walengwa wote tarajiwa.

"Utatoa huduma bora za uchunguzi wa magonjwa kwa lengo la kufikia zaidi ya wagonjwa milioni 1.7, udhibiti bora wa kuenea kwa saratani kwa kuongeza idadi ya wagonjwa wanaogundulika katika hatua ya awali kutoka asilimia 20 hadi asilimia 50 ya wagonjwa wenye uvimbe wa saratani, na kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya zahanati, pamoja na kuongeza elimu na uelewa wa saratani kwa umma kupitia vyombo vya habari na njia nyingine za mawasiliano," alisema.



Mmoja wa wafanyakazi wa Barrick Bulyanhulu akiuliza swali wakati wa ziara ya Mkuu wa Wilaya ya Kahama,Festo Kiswaga alipotembelea mgodi huo na kushiriki kuhamasisha zoezi la chanjo dhidi ya ugonjwa wa UVIKO 19 kwa wafanyakazi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ulinzi wa Ziwa Tanganyika waimarishwa

**Na Faustine Feliciane**

KAMPUNI ya huduma ya usambazaji kimataifa ya DHL imetoa msaada wa boti ya kisasa kwa Serikali kwa ajili ya kuimarisha ulinzi kwenye ziwa Tanganyika.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo yaliyofanyika mkoani Kigoma, Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Ndaki Mashimba, alisema msaada huo utaenda kuchochea uvuvi na utunzaji wa ziwa hilo lenye manufaa makubwa kwa wananchi wa Kigoma na maeneo ya jirani.

"Tunatambua kwamba sekta ya uvuvi imebadilika na kuwa shughuli muhimu ya kiuchumi badala ya kuwa suala la mazingira au viumbe hai, hivyo ni lazima tuilinde na kulinda maji yetu, msaada huu wa boti umekuja katika kipindi muhimu wakati huu wa mapinduzi ya uchumi wa bluu na kuunga juhudi za Rais wetu Samia Suluhu Hassan katika kuwaletea maendeleo wananchi wake." alisema Waziri Mashimba.

Alisema kuwa boti hiyo ya kisasa itatumika kwa kwa namna ilivyopangwa ikiwamo pia kuongeza nguvu ya ulinzi wa ziwa hilo.

Mkurugenzi Mtendaji wa DHL Express Tanzania, Paul Makolosi, alisema mchango wao wa boti ya ulinzi katika sekta ya uvuvi mkoani Kigoma utasaidia wavuvi kufanya kazi zao kwa ufanisi katika eneo la Ziwa Tanganyika ikiwemo kuvua samaki kwa usalama zaidi na kufikia malengo waliyojiwekea.

"Katika mioyo yetu tumekuwa na utaratibu wa kuwaunganisha watu kwa vitendo, DHL imekuwa ikifanya mambo mbalimbali kwa ajili ya kusaidia maisha ya wengi, sisi kama kampuni tunafanya kile ambacho kipo ndani ya uwezo wetu, sio tu kampuni ya kusambaza vifurushi lakini tumekuwa tukisaidia mambo mbalimbali kwa jamii inayotuzunguka," alisema Makolosi.

Aidha alisema umuhimu wa ziwa hilo kwa wakazi wa Kigoma na maeneo ya jirani umewagusa kutoa msaada huo wa boti kusaidia ulinzi na shughuri nyingine za uvuvi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa DHL kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, Fatima Sullivan, alisema kama kichocheo cha biashara na uwekezaji wenye athari nyingi kwa uchumi mpana wa kijamii na kiuchumi, DHL imeendelea kunufaisha biashara zinazolenga mauzo ya nje nchini Tanzania na huduma za wakati na sahihi.

# Serikali kununua magari ya wagonjwa 195

SERIKALI imesema kwa mwaka wa fedha 2021/22, itanunua magari ya wagonjwa 195 na kupelekwa kwenye halmashauri zote nchini ikiwamo Babati Vijijini.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Festo Dugange, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Babati Vijijini (CCM), Daniel Sillo.

Mbunge huyo alihoji lini serikali itapeleka gari la wagonjwa kwenye Kituo cha Afya Gidas.

Katika swali la msingi, Mbunge huyo alihoji lini serikali itasaidia ujenzi wa wodi ya mama na mtoto na chumba cha kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya Gidas.

Naibu Waziri Dugange alisema katika mwaka wa fedha 2021/22 serikali ilipeleka Sh. bilioni 1.04 kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Babati Vijijini kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri, Kituo cha Afya, nyumba ya mtumishi na ukamilishaji wa zahanati.

Alisema serikali inatambua uhitaji wa wodi ya mama na mtoto na chumba cha kuhifadhia maiti katika Kituo cha Afya Gidas.

"Kituo hiki kimeombewa fedha Hazina na ujenzi utaanza mara fedha zikitolewa," alisema.

Katika swali jingine la nyongeza, Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Munde Tambwe, alisema Manispaa ya Tabora ina idadi ya watu takribani 600,000 na kuna zahanati ambayo kinamama 10 hadi 20 wanajifungua kwa siku.

"Je, ni lini serikali itakuwa tayari kuipandisha hadhi zahanati na kuwa kituo cha afya na kuwawekea wodi ya wazazi pamoja na chumba cha upasuaji," alihoji.

Akijibu swali hilo, Dk. Dugange alisema serikali inafanya tathmini ya maeneo ambayo yana zahanati, lakini kuna idadi kubwa ya wananchi na umbali mrefu kutoka kituo cha afya hadi hospitali.

"Tutafanya tathmini kwenye hii zahanati ili kuona kama inakidhi vigezo ili ipandishwe hadhi na kuwa Kituo cha Afya," alisema.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akizungumza na Mbunge wa Viti Maalum Hawa Mwaifunga, Bungeni jijini Dodoma, **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**

## Vibali 618 vya ajira vilitolewa vyuo vikuu

WIZARA ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, imesema katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2018/2019 hadi 2020/2021, ilipata vibali vya kuajiri watumishi 618 katika vyuo vikuu vya umma 13.

Miongoni mwa watumishi hao wanataaluma ni 333 na waendeshaji ni 285.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga alitoa kauli hiyo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Thea Ntara.

Katika swali lake, Mbunge huyo alitaka kujua ni vyuo vikuu vingapi vimepewa fursa ya kuajiri watumishi wake.

Akijibu, Kipanga alisema vyuo vikuu kama zilivyo taasisi nyingine za umma huajiri watumishi baada ya kupata vibali vya ajira kutoka wizara yenye dhamana na utumishi wa umma na utawala bora.

Alisema pamoja na fursa hizo za kuajiri watumishi zilizotolewa, bado inaendelea na taratibu za kuwahamisha watumishi wenye sifa kutoka sehemu mbalimbali kujiunga na utumishi katika vyuo vikuu.

Alisema, serikali itaendelea kutoa vibali vya ajira katika vyuo vikuu kwa lengo la kuviongezea fursa ya kuajiri watumishi kadri ya upatikanaji wa fedha.




**Habari zote na Augusta Njoji**

## Zaidi ya mashauri 800 watumishi waliosimamishwa kazi hayajahitimishwa

BUNGE limeelezwa kuwa watumishi 836 waliosimamishwa kazi kuanzia mwaka 2015 hadi mwaka 2022, mashauri yao bado hayajahitimishwa.

Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Deogratius Ndejembi, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Mlimba (CCM), Godwin Kunambi.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji watumishi wangapi wamesimamishwa kazi tangu mwaka 2015 hadi 2022 ambao mashauri yao hayajaisha;

Akijibu swali hilo, Ndejembi alisema idadi hiyo ni watumishi waliosimamishwa kazi katika taasisi mbalimbali nchini ikiwamo Mamlaka za Serikali za Mitaa na Serikali Kuu.

Alisema watumishi hao ni miongoni mwa watumishi 1,477 waliokuwa wamesimamishwa kazi kwa kukiuka Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia nidhamu katika Utumishi wa Umma. "Mashauri haya yapo katika hatua mbalimbali za mamlaka za nidhamu ambazo ni waajiri mbalimbali na mamlaka za rufaa ambazo ni Tume ya Utumishi wa Umma, Tume ya Walimu na Ofisi ya Rais," alisema.

Aliwakumbusha waajiri na mamlaka za nidhamu kuongeza kasi ya kuhitimisha mashauri yaliyopo kwa kuzingatia taratibu za uendeshaji.

Awali, naibu waziri huyo alisema usimamizi wa nidhamu katika Utumishi wa Umma ni suala muhimu ambalo limeainishwa katika Sheria ya Utumishi wa Umma, Sura 298, Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Pia, alisema taratibu za uendeshaji katika utumishi wa umma za mwaka 2003, taratibu bora za nidhamu katika utumishi wa umma za mwaka 2007 na kanuni za kudumu katika utumishi wa umma za mwaka 2009.

Katika swali lake la nyongeza, Mbunge wa Arumeru Magharibi (CCM), Noah Mollel, alisema kulikuwa na watumishi wa darasa la saba waliosimamishwa na walikuwa wamefanya kazi kwa muda mrefu na baadaye hawakupewa kiinua mgongo wala chochote.

"Serikali inatoa kauli gani kwa watumishi hao ambao wametumikia taifa kwa kipindi kirefu kwa ujuzi huo wa darasa la saba," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Ndejembi, alisema watumishi wa darasa la saba walioajiriwa baada ya Mei 2004, serikali ilishatoa tamko ilimradi hawakughushi nyaraka zao walipewa muda hadi Desemba 2020 wawe wamejiendeleza ili kuendelea na ajira zao.

Pia, alisema watumishi ambao hawakujiendeleza mamlaka ilishatoa tamko kuwa washughulikiwe walipwe michango yao ya hifadhi ya jamii na hadi Desemba 2020, watumishi 1,191 walikuwa hawakujiendeleza na wanastahili kulipwa michango yao ya hifadhi ya jamii.



Ukurasa 12

Bao la wazee linavyoshika nafsi za vijana kutetea utamaduni


Ukurasa 13

Maradhi tata yanavyomsimamishia masomo kijana, ndoto kuwa daktari

Nipashe
TESA
Jumanne Aprili 12, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI




ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Darasa la mambo matano kutoka miaka miwili ya janga covid 19


Huduma za kukabili Uviko, katika hatua ya chanjo. **PICHA: MATADAO**

NI miaka miwili tangu Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza kuwapo mlipuko wa maradhi Covid-19 duniani.

Katika kipindi hicho, kunashuhudiwa kimataifa mambo matano ya kujifunza tangu kuanza janga hilo, ambayo yan amgusa kila mtu duniani aliko awe ameugua, ameshuhudia maradhi hayo au vinginevyo.

Mosi, kabla ya janga hilo kulipuka duniani, chanjo iliyowahi kutengenezwa kwa haraka sana kukabili majanga mengine, ilichukua miaka minne. Hata hivyo, ujio wa Corona ukaibua kasi ya utengenezaji chanjo mpya; wakati awali zilichukua miaka minne, safari hii ikawa miezi 11 tu.

Mara baada ya janga kuanza, watafiti walianza mbio ya kutengeneza chanjo ya kuwalinda dhidi ya Covid-19.

Baadhi ya kampuni za dawa zilitumia teknolojia ambazo matokeo yake hayajawahi kutumika kutengeneza chanjo iliyoidhinishwa kwa matumizi ya binadamu, kama MRNA.

Ni hatua inayotajwa kusaidia chanjo za Covid-19 haraka zaidi. Kwa kufanya hivyo, pia ilifungua mlango wa matibabu mapya ya utumiaji teknolojia namna hiyo.

Mchakato huo unafanya kazi kuunda mfumo wa kinga ya mwili unaoweza kujifunza na kuwa tayari kushambulia virusi vinavyofanana na Covid-19, iwapo utaambukizwa

**UTATA WA BARAKOA**

Pia, ikagundulika nchi nyingi zimebadili ushauri wa kuvaa barakoa na kuagiza zivaliwe katika mazingira fulani.

Karibu miezi minne baada ya mlipuko wa Covid-19 kutangazwa, Shirika la Afya Duniani (WHO) liliweka ujumbe kwenye mtandao wake 'Twitter' haiambukizwi kupitia hewa."

Wakati huo wataalamu wa WHO hawakuwa wakiwashauri watu kuvalia barakoa.

"Hatushauri utumiaji barakoa pengine ujiskie mgonjwa," aliongeza Maria Van Kerkhove, Kiongozi wa Kiufundi wa Covid-19.

Lakini, kile tulichojifunza tangu kuzuka kuanza kumebadilisha maoni hayo, WHO sasa inasema watu wanapaswa kuvaa barakoa kuwa sehemu ya kawaida ya maisha ili kuwa karibu na watu wengine.

Sasa inakiri ushahidi unaongezeka kwamba Covid-19 haiambukizwi tu kupitia matone makubwa ya mate au kamasi zilizoko hewani kwa muda mfupi baada ya mtu kukohoa au kupiga chafya, au kwa kugusa sehemu iliyo na virusi.

WHO sasa inasema, inaweza pia kuenea kupitia chembe ndogo zaidi ambazo zinaweza kubaki kwenye hewa kwa muda mrefu zaidi ikabadilisha ushauri wake na kusema kwamba Covid inaambukizwa kupitia hewa

**UTATA WA HEWA**

Katika tahariri, Jarida la Matibabu la Uingereza lilisema: "Watu wanapokaribiana wana uwezekano mkubwa wa kuambukizwa virusi kwa kuvuta hewa kuliko kuruka hewani kwa matone makubwa ya mate yanayotua machoni mwao, puani, au midomoni."

Utafiti huo ukapata ushahidi wa watu waliokuwa kwenye

**INAENDELEA UK.14**

ELIMU

NA ANTHONY GERVAS, MWANZA

# Bao la wazee Mwanza linavyoshika nafsi za vijana kutetea utamaduni

- Babu wa miaka 92 ajigamba yeye ni tishio
- Haijui shule, hisabati zake ana uweledi

BAO ni mchezo wa kitamaduni au kimila kutokana na kabila lenyewe. Kila kabila lina aina yake ya kucheza, lakini wazee wa jamii ya Wasukuma nao hucheza bao lao la kienyeji kwa aina yao.

Hivi sasa bao hilo huchezwa hata na vijana, tofauti na wazee ambao zamani walikuwa wakicheza na vijana kutoruhusiwa. Sasa, vijana wamekuwa wanajichanganya na wazee kufurahia mchezo huo kama ilivyo michezo mingine. Wengine hucheza bao linaloitwa la kiswahili.

Wazee ni raslimali kubwa ya taifa na kokote duniani ni muhimu,ambao mchango wao wa maoni, ushauri,mipango ya shughuli za maendeleo una nafasi yake, pia hutoa elimu dunia kwa vijana kufuata maadili mema.

Katika Wilaya ya Magu mkoani Mwanza, kata ya Kisesa na Wilaya ya Misungwi kata ya Fela, wazee wa kabila la wasukuma wameamua kuanzisha vikundi vya kushindana mchezo wa bao hilo la kitamaduni au mila wakieleza malengo yao.

Hivi karibuni wazee hao wa pande mbili, walicheza shindano hilo ambalo Kisesa waliibuka mabingwa wa mabao nane dhidi ya saba ya wazee wa Fela.

Mchezo huo ulichezwa saa tano kuanzia saa sita hadi saa 11 jioni kwenye kiwanja cha kata ya Kisesa, wakiwepo mashabiki wa pande zote wa kabila hilo na wananchi wengine watazamaji.



Anayecheza bao ni mzee Aman Karume, kutoka kata ya Fela Misungwi na Mzee Maliganya (kulia ) kutoka kata ya Kisesa Magu,wakizungukwa na wazee wengine mashabiki wao mchezoni.
**PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS**

### MZEE KARUME

Mzee Amani Karume, ni mkazi wa kata ya Fela wilayani Misungwi, mwenye umri miaka 92, lakini bado ni mjuzi wa kucheza bao la kijadi, akieleza kuwa lengo lake ni kuimarisha utamaduni huo, mila za bao hilo katika jamii hiyo na kuondoa mawazo ya uzee, akiongeza ujuzi wa kuhesabu kichwani mwake.

Vile vile anafafanua kwamba hali hiyo itamsaidia kujiepusha na maisha ya kukaa tu na kupata fikra za kwenda kwenye vilabu kulewa pombe, wakati akili yake hivi sasa akicheza bao inachangamka, akifafanua ubongo haugandi kulingana na jinsi anavyokuwa akifanya mazoezi kama hayo.

"Mimi nacheza bao, lakini sikusoma darasani, sikuwahi kwenda shule, lakini hesabu kichwani niko vizuri, mzee aliyesoma nina uwezo wa kumshinda mchezoni. Sikusoma hata ile elimu ya watu wazima, hadi sasa nina wajukuu 50 na vitukuu saba," anasema Mzee Karume.

> "Mimi nacheza bao, lakini sikusoma darasani, sikuwahi kwenda shule, lakini hesabu kichwani niko vizuri, mzee aliyesoma nina uwezo wa kumshinda mchezoni.

Anasema alianza kucheza akiwa kijana mdogo na sasa ujuzi alio nao ni mkubwa pamoja na kuzeeka zaidi, bado ni fundi kimchezo, hesabu zake hazijafeli na ndiyo maana wazee wenzake wamemshirikisha mashindano hayo ambayo safari yake inaanzia ngazi ya kata, wilaya, mkoa hadi wafike taifa.

### SHABIKI WAO AELEZEA

Mshabiki na mchezaji wa mchezo huo kutoka wilayani Misungwi, James Ngonda, anaelezea faida za kuanzisha shindano hilo ni kuinua vipaji vya wazee, kudumisha utamaduni wa wasukuma kupitia bao, kuwaweka pamoja kwenye upendo, uhusiano na kushirikiana kutatua changamoto zao za maisha.

Aidha kusaidiana katika shida na raha ikiwemo misiba, sherehe na shughuli zingine za maendeleo ya kijamii zilizopo, kwani uzee siyo dhambi wala mkosi, hivyo kuna haja ya jamii kuwaunga mkono wanapofanya jitihada zao binafsi za kimaisha.

Shabiki Ngonda anaeleza kwamba, wachezaji wake wanapata raha kama walivyo wachezaji wengine wa muziki, wakisakata ngoma na burudani zingine duniani, ni vyema wakapewa kipaumbele cha kuimarisha utamaduni huo.

Fela anasema atajipanga kulipa kisasi cha mabao waliyofungwa na Kisesa katika mchezo wa marudiano, kikubwa ni kuomba uzima siku ile itimie waweze kukutana na wapinzani wao.



Mratibu wa shindano hilo la bao, Benjamin Toboka.

### MRATIBU MASHINDANO

Mratibu wa shindano hilo, Benjamin Toboka, anasema machi mwaka huu, wanalikutana tena wazee wa Misungwi na Magu kushindania mbuzi dume, ambaye baada ya kumalizika mchezo alichinjwa na kuliwa kitoweo na wazee wa pande zote ikiwa ni ishara ya upendo.

Kwa mujibu wa Toboka, ni mchezo wa marudiano baina ya Kisesa na Fela, unaowawezesha kujipima kwenda kucheza shindano lingine katika kata, ili kujiandaa kushiriki kwenye ngazi ya wilaya ya Nyamagana.

### CHANGAMOTO ZAKE

Anafafanua changamoto zinazowakabili kwa sasa kikundi chao, ni ukosefu wa fedha za kusafiri kwenda sehemu nyingine kushindana kama vile nauli na chakula,sasa anaomba michango ya wadau wawasaidie.

Hata hivyo hivi sasa wamekuwa wakichanga gharama za usafiri na chakula wao wenyewe jambo ambalo anasema linawakwamisha kufikia malengo na ndoto za wazee hao,wanaojipambanua kuupenda ujuzi wao.

"Bado tunakabiliwa na changamoto ya gharama za usafiri na chakula, tunaposafiri kwenda kwenye mashindano kata zingine, wadau wetu tunaomba watuunge mkono ili tuweze kufikia malengo tusikate tamaa," anasema Benjamin.

Bao lina heshima yake kila kabila kwa wazee, huburudika na kujadili maisha yao, tofauti na michezo ya vijana kama karata au 'pool' linalowakusanya vijana wa rika zote wakiwemo wenye tabia mbaya, ikiwemo wezi.

Lakini kwenye burudani hiyo maadili yanatawala, hata kuwakanya wasiokuwa na maadili waendane na maisha ya watu wenye tabia njema, pale wanapoenda kinyume na utamaduni au mila.

Katika historia ya jamii ya Wasukuma tawala mbalimbali za watemi hapo zamani wazee walipumzika baada ya kazi na kucheza bao kwa ushirikiano aidha na majirani wa vitongoji vingine, ikibidi kushindana, ndiyo ilikuwa furaha yao enzi hizo.

Miiko na mila zetu za kila kabila bado muhimu, isipokuwa ambazo zinaumiza katika maisha,mfano kabila la Wamasai wamekuwa kielelezo cha nchi, kwa kutobadilisha asili yao.

ELIMU

NA MARCO MADUHU, SHINYANGA

# Maradhi tata yanavyomsimamishia masomo kijana, ndoto kuwa daktari

• Hatembei, pia maumivu makali • MNH: Kupona tiba India Sh. Mil. 40/- • Baba mzazi: Tuko kienyeji, kuna nafuu • Shuleni: Tumuombee, haki yake bado iko

HUJAFA hujaumbika, hasa ndio msamiati sahihi kwa hali inayomtokea mwanafunzi Peter Emmanuel (19), aliyekuwa akisoma kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari Ngokolo katika Manispaa ya Shinyanga, aliyeacha masomo, baada ya kuugua maradhi ya mgongo hata kuangukia kwenye ulemavu.

Peter anasimulia mkasa mzima wa maradhi yake na namna yalivyoanza kwamba, alipofika darasa la saba mwaka 2017, mgongo ulianza kumuuma na alipoingia kidato cha kwanza 2018 hali hiyo iliendelea.

Anasema ndicho kilichomtawala hadi kufika kidato cha pili ikichukua sura mbaya zaidi, hata kuingia hatua kidato cha tatu, ngazi ambayo amesoma kidogo akashindwa kuendelea na masomo na ndoto zake kuwa daktari zikaanza kufifia.

Kijana huyo anasimulia mkasa wake, kwamba alipofika kidato cha tatu, miguu yake ilianza kuisha nguvu na hata kufika hatua ya kushindwa kutembea kabisa, huku akipata maumivu makali kwenye mgongo. Ni hali iliyomfanya abaki nyumbani kushughulikiwa matibabu.

"Mimi kwa sasa nimeacha shule sababu ya kupata maradhi ya mgongo. Niliacha nikiwa kidato cha tatu mwaka (2020) na mwaka jana ningekuwa nimemaliza elimu yangu ya kidato cha nne na ndoto zangu nilitaka kuja kuwa daktari, lakini sijui kama nitarudi tena shule ili kutimiza ndoto zangu," anasema Emmanuel.

Anafafanua kwamba hivi sasa, baada ya kushindwa kupata tiba hospitalini na kurudi nyumbani, ameongezea na tiba za asili hali anayosema walau inamuwezesha kuanza kutembea baada ya kupatiwa tiba za asili, akitumia magongo.




Mwanafunzi Peter Emmanuel, akisimama kwa msaada wa magongo. **PICHA: MARCO MADUHU**

#### NJIA PANDA ILIVYO

Ni hali ambayo Peter anaieleza kwamba inampa matumiani ya kurudi masomoni, lakini bado mgongo unamsumbua kutokana na wazazi wake kukosa pesa za kumuwezesha kufanyiwa upasuaji nchini India.

Baba wa mwanafunzi huyo, Emmanuel Makomba, anasema mtoto wake alizaliwa bila ya kuwa na tatizo lolote, lakini alipofika darasa la saba ndipo akaanza kulalamika kuwa anaumwa mgongo.

Anasimulia kwamba alipoingia kidato cha kwanza akaendelea kulalamika kuwa maumivu yanazidi, ndipo wakaanza kumpatia matibabu, lakini alipofika kidato cha tatu, hali yake ikawa mbaya zaidi hata akashindwa kutembea na kulazimika kusimamisha masomo, ili atibiwe.

"Mtoto wangu kwa sasa hasomi tena shule alikomea kidato cha tatu mara baada ya kupata maradhi ya mgongo, na kwa mujibu wa madaktari kutoka Muhimbili. Mgongo wake umepinda mara tatu na ameshakuwa mlemavu tayari," anasema Makomba.

Anafafanua kuwa madaktari hao wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, walimwambia ili mtoto wake apone kabisa, anapaswa kupelekwa nchini India na itawagharimu kiasi fedha Sh. milioni 40, lakini kwa kukosa uwezo, ikabidi warudi nyumbani Shinyanga na kuanza kumtibu kwa njia za asili wakilipa Sh. 125,000 kila mwezi kwa dozi ya miezi sita.

"Awali mtoto wangu kabla ya kupata matibabu hata kidogo, hali yake ilikuwa mbaya zaidi alikuwa hawezi hata kutembea.

"Lakini kwa sasa, angalau anatembelea magongo na bado anaendelea na matibabu ya asili sababu tulikosa fedha Sh. milioni 40 za kumpeleka nchini India kufanyiwa upasuaji," Mzee Makomba.

> Awali mtoto wangu kabla ya kupata matibabu hata kidogo, hali yake ilikuwa mbaya zaidi alikuwa hawezi hata kutembea.

Mama mazazi wa mwanafunzi huyo, Joyce Ntumali, anawaomba wadau, taasisi na mashirika mbalimbali, kumsaidia mtoto wao kiasi hicho cha fedha Sh.milioni 40, ili akapate matibabu nchini India, arudi shule akatimize ndoto zake.

"Sisi hatuna uwezo kabisa wa kumpeka mtoto wetu kwenye matibabu nchini India baada ya kuzunguka karibia hospitali zote hapa nchini na kuambiwa hadi apelekwe India ndipo atapona.

"Ikabidi turudi tu nyumbani na kumpatia matibabu ya asili, lakini akifanyiwa upasuaji wa mgongo nina imani atapona kabisa na kurudi shule," anasema Ntumali.

Anaendelea "Tiba za Asili ambazo tunampatia, zenyewe zinaonyesha matumaini ya miguu yake kupata nguvu na kutembea kwa kutumia magongo, lakini tatizo la mgongo bado lipo pale pale sababu hawezi hata kunyooka na kutembea huku akiwa ameinama hadi afanyiwe upasuaji," anaongeza Ntumali.

Mkuu wa Shule ya Sekondari Ngokolo Manispaa ya Shinyanga Malale Masali, anasema Mwanafunzi huyo alikuwa akisoma shuleni hapo, lakini aliacha masomo kidato cha tatu mara baada ya kupata maradhi ya mgongo.

Anasema kwa taratibu za elimu Mwanafunzi akiacha masomo sababu ya maradhi, akipona anaweza tena kurudi shule na kuendelea na masomo yake kwa kukariri darasa kwa kuanzia kidato alipokomea.

Anafafanua kuwa Mwanafunzi huyo Peter Emmanuel, bado ana nafasi ya kuendelea na masomo yake endapo akipona na kutaka kurudi shule, ambapo wazazi wake wataandika barua ya kuomba nafasi tena pamoja na kuambatanisha nyaraka zote za matibabu.

***• Kwa mtu yeyote anayeguswa kumsaidia mwanafunzi huyo, awasiliane na baba yake mzazi Emmanuel Makomba kwa simu: (+255) 755 912724.***

# Darasa la mambo matano kutoka janga la covid 19

INATOKA UK.11

na kufafanua:

"Ndio sababu inayowezekana kueneza na sababu kwa nini baa na migahawa ya ndani ni hatari sana."

Kunawa mikono na kuosha maeneo yanayoguswa na wengi, inatajwa ni jambo la msingi zaidi kuvaa barakoa na kuwa katika chumba chenye nafasi ya kuingiza hewa safi.

**OFISI MAJUMBANI**

Mlipuko wa Covid umetoa uzoefu kwamba inawezekana kutumia muda mrefu kwenye simu za video, kuungana kikazi na ndivyo mamilioni ya watu duniani walilazimika kufanya kazi nyumbani, kujinusuru na janga la corona.

Ni kitu ambacho hakikuwezekana kiufundi miaka michache iliyopita, lakini Covid imeonyesha kwamba inawezekana. Ni hali inayoweza kuwabadilisha mamilioni jinsi wanavyofanya kazi.

Kampuni kubwa ya mitandao ya kijamii ya Twitter iligonga vichwa vya habari kote duniani mnamo Mei 2020 ikisema:




Tukio la kupokea dawa za chanjo nchini. **PICHA: MTANDAO**

"Wafanyakazi wa 'Twitter' sasa wanaweza kufanya kazi wakiwa nyumbani milele... miezi michache iliyopita imethibitisha kuwa tunaweza kuifanya kazi hiyo."

Pia, kampuni ya Facebook, ilitoa tangazo kama hilo mapema mwaka huu, huku kura ya maoni ya kampuni 1,200 iliyofanywa na kampuni ya utafiti ya Enterprise Technology, ikaonyesha asilimia ya wafanyakazi ambao wanaofanya kazi zao nyumbani, waliongeza tija mara mbili, mnamo mwaka 2021.

Katika uchunguzi wa kimataifa wa watu zaidi ya 200,000 katika nchi 190, asasi ya Boston Consulting nayo iligundua kuwa asilimia 89 ya walioajiriwa walikuwa na uwezo wa kufanya kazi nyumbani wakati fulani.

**CORONA VS JAMII**

Inatajwa watu kutoka jamii zisizo na uwezo waliathiriwa sana na Covid -19, mfano ukiangukia Uingereza, utafiti uliofanywa na Benki ya Biobank ya Uingereza uligundua sehemu iliyoathiriwa zaidi ya nchi.

Asilimia 11.4 ya walioambukizwa na Covid, ni walioko katika maeneo ya yenye kipato cha chini na kati yao 7.8 ni kutoka makazi duni.

Huko New York, Marekani data za mwaka 2020 zilionyesha Wahispania na Wamarekani weusi ilijumuisha asilimia 34, pia asimilia 28 ya vifo vyote vya Covid.

**KITENDAWILI CHA KUISHA**

Kigumu ni bado hakuna uhakika janga la Covid-19 litaisha lini. Mtazamo uliopo ni kwamba, iwapo watu wengi watapata usugu dhidi ya Covid 19, uambukizaji ugonjwa huo au chanjo ya virusi itakuwa tishio zaidi.

Imebainika kuwa mwitikio wa mifumo ya kinga iliyopo inapungua kadri muda unavyosonga, ndiyo maana nchi zinazojiweza zinazindua mpango wa chanjo ya nyongeza.

Kumrejea msomi, Profesa Shabir A Madhi, Mkuu wa Kitivo cha Sayansi ya Afya na profesa wa chanjo katika Chuo Kikuu cha Witwatersrand, Afrika Kusini, anasema mwitikio wa kinga baada ya kuambukizwa au chanjo huchukua takriban miezi sita hadi tisa.

Anafafanua, virusi vimebadilika haraka na aina nyingine ya corona, inayoweza kuambukizwa na kuibuka na huenda ikawa vigumu kudhibitiwa kwa chanjo.

• ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***

## WANENAVYO MALENGA

### TUTALIA HATA LINI?

Tutalia hata lini, machozi yenye huzuni?
Na wenyewe duniani, twatiana msambweni?
Vyombo vya barabarani, kutuweka kaburini?
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Mtu kufa ni huzuni, hapa kwetu duniani,
Haiswihi asilani, msiba tuwe rahani,
Vipo vingine lakini, vinayo matumaini,
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Mapenzi ya Maanani, watu tufe uzeeni,
Mambo haya ujanani, huchoma sana moyoni,
Miaka ya kitabuni, kutoweka mikononi,
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Hata na Yesu zamani, lipokuwa ujanani,
Likuwa kubwa huzuni, kutoweka duniani,
Japo badaye amani, lifufuka yu mbinguni,
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Huu mkuki moyoni, vifo vya barabarani,
Twajitia hatarini, tunapokuwa njiani,
Mtu uwe ni makini, unaponzwa na mhuni,
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Taarifa redioni, na nyingine runingani,
Ajali nyingi nchini, uzembe u kileleni,
Tungelikuwa makini, ajali ngekuwa chini,
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Sikia masikioni, ni miaka hamsini,
Kasombwa barabarani, huyu baba wa nyumbani,
Watoto kindagateni, wanabakije jamani?
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Wa miaka ishirini, afikie themanini,
Wa miaka hamsini, hata afike tisini,
Tena afe kwa amani, ametulia nyumbani,
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Iweje barabarani, tuwe kama mtegoni?
Kila siku tusaini, kama twenda hukumuni?
Tupinduke milimani, tena hata mabondeni?
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

Adui wa duniani, kwetu tulo safarini,
Sisi wenyewe jamani, umakini uko chini,
Tunafanya mambo duni, twajitia hatarini,
Tuamkeni jamani, kifo kije kwa amani.

**Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

### NCHA YA PANGA HATARI

Walikuwa wanapigwa, sasa nao wanapiga,
Kwa jinsi walivyotegwa, wamerogwa wan-
aroga,
Sisi ndio twavurugwa, uchumi wauvuruga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga
hatari.

Mtu kama asukumwa, huku analegalega,
Awe kama ni mtumwa, humuachi akizuga,
Achokwa kuumwaumwa, naye aonesha swaga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga
hatari.

Kushinda kitu kingile, ila waweza kupiga,
Kwa wababe hiyo shule, lazima yawavuruga,
Ninachowazia zile, nguvu zao wakipiga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.
Mafuta bei zapanda, visima wamevuruga,
Bei zitazidi panda, na maisha kuvuruga,
Wapende bila kupenda, waache kutegatega,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.

Jamaa wameumia, kwa jinsi walivyowapiga,
Kazi kusikilizia, jinsi nao watapiga,
Panya watamvamia, kwa mabomu ya kutega?
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.

Vipi mnazungumza, huku mwazidi kupiga,
Amani mnaiwaza, au mnazugazuga?
Jamani mwatumaliza, maisha yanatupiga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.

Huko wanatafutana, ni vipi wamewapiga,
Kwa jinsi walijiona, hawawezi wakapiga,
Sasa vema wakaona, waziache zao swaga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.

Jazba zenu punguza, uchumi mwauvuruga,
Wapambe mkikoleza, mnazidi kuvuruga,
Vita msijeeneza, wenzenu mkatutoga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.

Amani tena amani, haifiki kwa kupiga,
Lazima kaa mezani, mpange mazagazaga,
Masoja wende kambini, waache kupigapiga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.

Yetu macho tunaona, jinsi wanapigapiga,
Hofu hasa twaiona, mkubwa wanampiga,
Ataibuka twaona, kuchakaza kwa kupiga,
Chonde chonde nyie watu, ncha ya panga hatari.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**





## Wenye dhamana kusimamia walimu wapewa maelekezo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

SERIKALI imewataka watendaji wenye dhamana ya kuwasimamia walimu kusikiliza changamoto binafsi zinazowakabili.

Imesema lengo ni kuepuka kuwasababishia msongo wa mawazo unaochangia kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Dk. Grace Magembe, ndiye aliyetoa maelekezo , alibainisha hayo wakati akifunga mafunzo elekezi ya wajumbe wa Kamati za Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) za Wilaya kutoka Kanda ya Kaskazini na Kusini.

Dk. Magembe alisema Serikali imelenga kuwasaidia walimu kwa kuwawekea mazingira mazuri ili waweze kutoa huduma bora kwa wanafunzi, hivyo watendaji wenye dhamana ya kuwasimamia hawanabudi kuelekeza nguvu zao katika kutatua changamoto za walimu.

"Unakuta mwalimu ana shida anahangaika lakini akifika kwa kiongozi wake hasikilizwi badala yake humfokea na kumfukuza," alisema Dk. Magembe.

Alisema jambo hilo linafanya watumishi kuwa na msongo wa mawazo, ikiwemo kukata tamaa na mwisho anaingia kwenye makosa ya kinidhamu na hatimaye anafukuzwa kazi.

Alisema pamoja na kwamba sheria, kanuni na taratibu zipo na ni lazima zizingatiwe, ni muhimu pia wenye dhamana kutumia utu, hekima na busara ili kuwasaidia walimu kutoingia katika makosa ya kinidhamu badala ya kukaa na kusubiri wafanye makosa ili wawachukulie hatua.

"Ninyi TSC mmepewa dhamana kubwa kushughulikia masuala ya utumishi wa walimu, wasikilizeni walimu na wasaidieni kutatua changamoto zao,"alisema Dk Magembe.

"Kuna wengine unaweza kukuta wamechanganyikiwa kabisa na kukata tamaa lakini kumbe ukiwasikiliza utakuta tatizo ni dogo tu, ambalo unaweza kushauriana na mkurugenzi wa halmashauri kulipatia ufumbuzi,"alisema

Naibu Katibu huyo alisema katika kipindi cha mwaka mmoja tangu aingie madarakani, Rais Samia Suluhu Hassan, amefanya kazi kubwa ya kuboresha elimu ikiwemo kujenga madarasa zaidi ya 15,000, kuajiri walimu zaidi ya 6,900 ikiwemo kupandisha madaraja walimu 126,346 na kuwabadilishia vyeo walimu 11,363.

"Hivyo Kamati hizo nazo zina wajibu wa kuunga mkono juhudi hizo kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi,"alisema

Alifafanua kuwa dhamira ya serikali ni kuhakikisha wanafunzi wanafundishwa vizuri hivyo ni lazima TSC ihakikishe kuwa walimu wanatulia kwenye vituo vyao vya kazi na wanafanya kazi wakiwa na amani badala ya kuondoka vituoni kwenda kuhangaikia masuala yao ya kiutumishi.

Hata hivyo alisema TSC inatakiwa kuwa daraja kati ya walimu na ofisi mbalimbali za serikali zinazoshughulikia walimu na kufanya ufuatiliaji wa karibu ili kila mwalimu anayewasilisha shida yake TSC aweze kupatiwa majibu kwa wakati.

# Biteko atatua mgogoro wa wachimbaji wadogo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Madini, Dk. Doto Biteko, ametatua mgogoro wa wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu katika kijiji cha Nayu kata ya Dabalo wilayani Chamwino mkoa wa Dodoma.

Mgogoro huo uliodumu kwa zaidi ya mwaka mmoja ulitokea baada ya wachimbaji wadogo kugundua madini ya dhahabu katika Mlima wa Nayu uliopo ndani ya hifadhi za misitu ambapo mwekezaji, Salehe Mohamed, alikata leseni ya uchimbaji mdogo wa madini katika eneo hilo.

Inaelezwa kuwa kijiji cha Nayu kina leseni 16 ambapo mwekezaji ana leseni nane na wanakijiji wana leseni nane ambazo zinamilikiwa kihalali kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa na serikali.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara na wachimbaji wadogo wa madini, Dk. Biteko alisema Wizara ya Madini inatoa leseni za uchimbaji katika maeneo mbalimbali, pale inapotokea leseni ipo ndani ya hifadhi za misitu ni lazima mmiliki apate kibali kutoka Wakala wa Misitu Tanzania (TFS).

"Sisi Wizara ya Madini tunatoa leseni kwenye maeneo yenye madini, lakini ukitaka kuchimba kwenye hifadhi za misitu lazima upate kibali kutoka TFS ili uchimbe kwa utaratibu ambapo wataalam wa misitu watakagua eneo na watakupa kibali cha tathmini ya athari za mazingira ili kuhakikisha mazingira yanabaki salama," alisema Dk. Biteko.

Aidha, Dk. Biteko alisema ni muhimu mwekezaji wa madini ya dhahabu katika kijiji hicho Salehe Mohamed kujenga mahusiano mazuri na wanakijiji aliowakuta katika eneo hilo ili afanye kazi kwa ushirikiano.

Dk. Biteko alisema Rais Samia Suluhu Hassan anataka kuona wachimbaji wadogo wa madini wananufaika na rasilimali zilizopo nchini, anataka kuwaona wachimbaji wadogo wanatoka kwenye uchimbaji mdogo kwenda wa kati na hatimaye kuwa wachimbaji wakubwa.

"Mwenyezi Mungu amewapa bahati ya kuwa na madini katika eneo lenu, niwaombe mchimbe madini haya kwa kupendana na kushirikiana, madini yawaunganishe acheni mambo ya kufitiniana na kuleteana majungu chimbeni kwa ushirikiano," alisisitiza Dk. Biteko.

Aidha, alimuagiza Mkuu wa Wilaya ya Chamwino, Gift Msuya na Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Dodoma, Chagwa Marwa kufungua soko la madini katika kijiji cha Nayu ili kuwarahisishia wachimbaji wadogo mahali pa kuuzia na kusaidia kijiji kupata tozo kutoka kwenye madini yaliyopo kwenye eneo lao.

Mkuu wa Wilaya Msuya, alisema migogoro mingi inayotokea katika eneo hilo inasababishwa na ukosefu wa elimu kwa wachimbaji wadogo, ambapo mara nyingi wakigundua madini wanaanza kuyachimba bila kufuata sheria na utaratibu.

Mbunge wa Chamwino ambaye pia ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora), Deogratius Ndejembi, alimpongeza Waziri Biteko kwa kukubali kuongozana naye ili kutatua mgogoro huo uliodumu kwa muda mrefu.



MWENYEKITI wa Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) Adam Kimbisa, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma juzi kuhusu mpango wa bunge la Afrika Mashariki kuhamasisha wananchi kuhusu mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. **PICHA: PAUL MABEJA**

# W/biashara waonyeshwa fursa za EAC

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAFANYABIASHARA nchini wametakiwa kuchangamkia fursa za kibiashara ambazo zinapatikana katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na kuacha kuwa walalamikaji.

Mwenyekiti wa Wabunge wa Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA), Adam Kimbisa, alibainisha hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari na wadau wa biashara katika majadiliano kuhusu Mtangamano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kimbisa, alisema kwa sasa kupitia EAC kuna fursa nyingi za kibiashara, lakini bado wafanyabiashara wa kitanzania hawajawa na mwamko wa kuchangamkia fursa hizo.

Kimbisa alisema fursa nyingine ambayo wafanyabiashara wa Tanzania wanatakiwa kuichangamkia ni kutembelea nchi jirani kama ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kukutana na wafanyabiashara wa kule kwa lengo la kubadilishana mawazo ya kibiashara.

"Kwa nchi ya Tanzania kusema ukweli Rais, Samia Suluhu amekuwa mstari wa mbele zaidi katika kufungua fursa za kibiashara katika nchi mbalimbali anapokwenda kufanya ziara.

"Na kwa nafasi hiyo basi wafanyabiashara wa Kitanzania wanatakiwa kuchukua hatua za makusudi ili kuhakikisha wanaunganika na wafanyabiashara wenzao huko duniani kwa nia ya kuangalia ni fursa gani kwao zinaweza kuwa na umuhimu kwa nia ya kuwekeza," alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo ,Wafanyabiashara hawatakiwi kuendelea kuwa watazamaji,washangiliaji na walalamikaji na mfanyabiashara asione hasara kusafiri kwenda nje kwa nia ya kutafuta fursa kwa kutoka kwenda kuwatembelea wafanyabiashara wengine.

Aidha, Kimbisa alisema kuwa soko la pamoja limefungua fursa mbalimbali kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema hatua hiyo ilihitaji hatua mbalimbali za kuchukuliwa na Jumuiya kwa pamoja na kila nchi mwanachama zilitakiwa kurekebisha au kutunga sheria mbalimbali kwa ajili ya kuwezesha kutekeleza itifaki ya soko la pamoja.

Katika hatua nyingine, alibainisha baadhi ya mafanikio ya Jumuiya hiyo kuwa ni utekelezaji wa umoja wa forodha na soko la pamoja.

Kuanzishwa kwa vituo 15 vya huduma za pamoja za mipakani, himaya moja ya forodha, kuongezeka kwa biashara ya ndani ya himaya kutoka dola 1.6 bilioni mwaka 2005 mpaka dola 3.2 bilioni mwaka 2020 na kuongezeka kwa mtaji na uwekezaji katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Pamoja na kuwepo kwa baadhi ya mafanikio pia alizitaja baadhi ya changamoto zinazochelewesha Mtangamano wa Jumuiya hiyo.

Chagamoto hizo ni kuchelewa kurekebishwa kwa baadhi ya sheria katika nchi wanachama, kuchelewa kutungwa kwa baadhi ya sheria za jumuiya, kuwepo kwa vikwazo vipya visivyo vya kiforodha.





# Wazazi wahamisha watoto shule wakihofia imeuzwa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UVUMI uliokuwa umezuka mitaani kwamba Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi (CCM), inakusudia kuiuza Shule ya Sekondari Meta iliyopo jijini Mbeya, umesababisha asilimia kubwa ya wazazi kuwahamisha watoto wao kwenye shule hiyo.

Hali hiyo inadaiwa kuifanya shule hiyo kuwa na idadi ndogo ya wanafunzi hali ambayo inasababisha kushindwa kujiendesha vizuri na hata kushuka kitaaluma tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambayo ilikuwa miongoni mwa shule bora.

Kutokana na hali hiyo, uongozi wa Jumuiya hiyo umewaondoa hofu wazazi na walezi kuwa haina mpango wa kuiuza wala kuibadilishia matumizi na kwamba unakusudia kuiboresha ili irejee katika hali yake ya kawaida.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Wazazi wa Chama cha Mapinduzi Taifa, Gilbert Kalima, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipofanya ziara ya kukagua miradi ya jumuiya hiyo katika Jiji la Mbeya ambapo aliwatoa hofu wazazi na walezi wanaokusudia kuwaondoa watoto wao.

Alisema kwa sasa Jumuiya hiyo inakusudia kuwatumia wanafunzi wachache waliopo kuitangaza shule hiyo kwa kuhakikisha wanafaulu vizuri ili kuwa chachu ya wazazi wengine kupeleka watoto wao kwenye shule hiyo.

Alisema miundombinu ya shule hiyo ambayo ilikuwa imechakaa hasa madarasa na mabweni ya wanafunzi yataboreshwa ili kila mazingira yawe ya kuvutia kwa wanafunzi hao. "Hatuna mpango wowote wa kuiuza hii shule wala hatuna mpango wowote wa kubadili matumizi ya shule, wale wazazi wote ambao walikuwa na wasiwasi waondokane na uvumi huu hauna ukweli wowote," alisema Kalima.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Ally Bakari alielezea mikakati iliyopo kwa sasa ya kuboresha shule hiyo pamoja ili iwe na mvuto kwa wazazi na wanafunzi kama ilivyokuwa awali.

Alisema mbali na kuiboresha shule hiyo pia wanakusudia kulitumia eneo lililobakia katika shule hiyo kujenga shule ya msingi ya mchepuo wa kiingereza ili kuongeza wigo wa utoaji elimu katika shule hiyo na katika mkoa wa Mbeya.

Alisema wanafunzi watakaokuwa wanafaulu kutoka kwenye shule hiyo watakuwa wanatumika kama mabalozi wa kuitangaza shule hiyo na kuifanya kuwa kivutio zaidi kwa wananchi.

"Mabweni ambayo yamechakaa tuna mpango wa kuyaboresha na hata madarasa tutayaboresha, lengo letu ni kuifanya shule kuwa ya kuvutia na tutaifanya kuwa miongoni mwa shule bora katika mkoa huu," alisema Bakari.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya wazazi wa Chama hicho Mkoa wa Mbeya, James Mwampondele, alisema mbali na kuboresha shule hiyo pia wana mpango wa kufanya mazungumzo na Mamlaka ya Mapato (TRA) kuhusu madeni ambayo shule za Jumuiya hiyo zinadaiwa.

Alisema lengo la mazungumzo hayo ni kuangalia namna ya kulipa madeni ambayo wanadaiwa hasa yanayohusiana na mambo ya kodi na kwamba ikiwezekana wawe wanalipa kidogo kidogo.

Shule hiyo miaka ya nyuma ilikuwa na wanafunzi zaidi ya 2000 na ilikuwa miongoni mwa shule zenye idadi kubwa ya wanafunzi katika Mkoa wa Mbeya, lakini kwa sasa inadaiwa kuwa ina wanafunzi wasiozidi 200.



Mlezi wa Jukwaa la Kiuchumi la waandishi wa habari mkoa wa Mbeya, Ndele Mwaselela akizungumza na wanachama wa jukwaa hilo mwishoni mwa wiki ambapo aliahidi kusadia wanahabari hao kupata mikopo yenye nafuu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Viongozi dini waombwa uhamasishaji wa sensa

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIONGOZI wa Dini mkoani Mbeya wametakiwa kusaidia kuhamasisha wananchi kushiriki kwenye zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ambalo linatarajiwa kufanyika kuanzia Agosti 23, mwaka huu.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Tanzania Assemblies of God (TAG) Forest ya Kwanza jijini Mbeya, Thobias Tambikeni, alitoa ombi hilo wakati wa ibada maalumu ya kuliombea taifa na viongozi wake pamoja na kuombea taifa kuepuka majanga mbalimbali.

Tambikeni alisema wapo baadhi ya watanzania ambao wamekuwa wakitoa taarifa za kupotosha kuhusu zoezi hilo la sensa kwa kulihusisha na baadhi ya mambo jambo ambalo alisema viongozi wa dini wana wajibu wa kutoa elimu.

Alisema wapo baadhi ya watu wameanza kueneza taarifa za uongo mitaani wakidai kuwa lengo la sensa hiyo ni kutaka kujua idadi ya Watanzania waliochanjwa chanjo ya Uviko 19 jambo ambalo alisema halihusiani kabisa.

"Suala la kuhesabiwa hata kwenye vitabu vitakatifu limeandikwa maana hata Yesu alienda kuhesabiwa, sasa sisi binadamu wa kawaida kwanini tusihesabiwe? Naombeni tushirikiane kuwahamasisha wananchi ili wote tukashiriki zoezi hili," alisema Mchungaji Tambikeni.

Nao baadhi ya waimbaji wa nyimbo za injili walioshiriki mkutano huo waliunga mkono hoja ya mchungaji huyo wakidai kuwa zoezi hilo lina faida kubwa kwenye upangaji wa bajeti zake. Mmoja wa waimbaji hao, Ambwene Mwasongwe, alisema sensa inaisaidia Serikali kupanga mipango mbalimbali ya maendeleo akidai kuwa haiwezi kupanga mipango hiyo bila kujua idadi ya wananchi ambao inawahudumia.

Alisema elimu inatakiwa ianzie kwenye nyumba za ibada ili wanaoipata wasaidie kuwaelimisha wenzao ambao wapo mitaani wanakoishi ili nao wajue umuhimu wa zoezi hilo.

# Spika Tulia awakumbuka waandishi wa habari

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SPIKA wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Tulia Ackson, ameanzisha tuzo maalumu za umahiri wa waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya ambazo zinatarajiwa kufanyika kwa mara ya kwanza mwaka huu.

Dk. Tulia ameanzisha tuzo hizo kupitia taasisi yake ya Tulia Trust na zinatarajiwa kusimamiwa na taasisi hiyo kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za kihabari likiwemo Baraza la Habari Tanzania (MCT) na taasisi zingine.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa taasisi ya Tulia Trust, Joshua Mwakanolo, aliyasema hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu uanzishwaji wa tuzo hizo ambapo alisema waandishi wa habari watashindana kwenye makundi 12.

Aliyataja makundi hayo ni umahiri wa uandishi wa habari za elimu, habari za afya, habari za mazingira, habari za makundi maalumu, habari za maliasili na utalii, utamaduni na michezo na habari za siasa.

Aliyataja makundi mengine ni umahiri kwenye habari za watoto, habari za uchunguzi, habari za uchumi na biashara, habari za unyanyasaji wa kijinsia na tuzo za mwisho ni mpiga picha bora.

Alisema waandishi watakaoshiriki kwenye tuzo hizo ni wanaofanya kazi kwenye vyombo vya habari mbalimbali zikiwemo televisheni, redio, magazeti na vyombo vya habari vya mtandaoni.

"Habari zitakazoshirikishwa kwenye tuzo hizi ni zile ambazo ziliandikwa kuanzia Julai 2021 mpaka Julai 31 mwaka huu na kazi zitaanza kuwasilishwa Agosti mosi mwaka huu," alisema Mwakanolo.

Aidha alisema tuzo hizo zitakuwa endelevu na kwamba lengo la kuanzisha tuzo hizo ni kutambua mchango wa waandishi wa habari kwenye utendaji kazi wa shughuli mbalimbali za kijamii.

Vilevile alisema zawadi za washindi wa tuzo hizo zitatangazwa baadaye kwa maelezo kuwa kuna vitu vinaendelea kuboreshwa kwa kushirikiana na wadau.

Baadhi ya waandishi wa habari wa Mkoa wa Mbeya, walipongeza taasisi ya Tulia Trust kwa kuanzisha tuzo hizo wakidai kuwa zitakuwa chachu ya kuongeza umahiri kwenye utendaji kazi wao na kwamba tuzo hizo zitatumika kuhamasisha waandishi.

Esther Macha alisema waandishi wengi walikuwa wanashiriki tuzo zinazoratibiwa na Baraza la Habari la Taifa (MCT) pekee lakini kwa sasa wameongezewa eneo lingine la kushindanishwa.

"Mimi naamini Mkoa wetu una waandishi wengi wazuri, lakini ambao wamekuwa wakishiriki tuzo za kitaifa wamekuwa wakijitokeza wachache, sasa hii naamini itakuwa chachu ya kuongeza washiriki kwenye tuzo za kitaifa," alisema Esther.

Naye Sadam Sadick alishauri tuzo hizo kufanyika kwa kuzingatia usawa ili waandishi wote wafurahie na washiriki kwa maelezo kuwa ikitokea upendeleo baadhi ya waandishi wanaweza wakakosa ujasiri wa kushiriki.

## Othman ataka wenye mahitaji kusaidiwa

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amewataka wananchi kuendeleza mshikamano kwa kuwasaidia wenye hali duni kiuchumi katika kutimiza mahitaji yao ya kila siku hasa kipindi hiki cha mwezi mtukufu wa Ramadhani.

Othman alitoa wito huo alipofanya ziara ya kuwatembelea na kuwajulia hali baadhi ya wagonjwa, yatima na vizuka katika maeneo tofauti ya Mkoa wa Kusini Unguja akiwa katika mfululizo wa ziara maalumu mkoani humo.

Alisema kufanya hivyo ni muhimu katika kutarajia neema zitokanazo na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani ambao ni mwezi wa machumo ya thawabu na kufutiwa dhambi kwa kutenda mambo mema ya ibada ikiwamo kusaidiana na kuwatembelea wagonjwa.

Othman alisema kuendeleza mshikamano na kusaidiana miongoni mwa wanajamii pia ni kuendeleza jambo la ibada na kuifanya nchi kuwa na neema kutokana na umoja na mshikamano.

Aidha, alisema Mwezi wa Ramadhani ni muhimu pia kutumiwa kupata elimu itokanayo na mafunzo ya mwezi huo na kuitaka jamii kujilinda na kujiepusha na hasara ya kuwa na elimu isiyo na faida, jambo ambalo linapaswa kuepukwa na jamii kwa kuacha mambo maovu.

Othman pia aliitaka jamii kuyatumia mafunzo yatokanayo na Mwezi Mtukufu wa Ramadhani kwa kuombeana dua za kuepushwa na kuingia katika mambo yasiyofaa ambayo yamekatazwa na Mungu.

Alisema kutembeleana katika kipindi cha Ramadhani ni mila na desturi njema miongoni mwa wanajamii ambayo huzaa utamaduni bora, hivyo kuwapo utambulisho mzuri ndani ya jamii husika.

Wagonjwa waliotembelewa na Makamu wa Kwanza wa Rais walimshukuru kwa kuwa na utamaduni huo na kwamba ni jambo linalowapa faraja kubwa kwamba viongozi wapo pamoja nao.

Othman katika ziara hiyo alitembelea na kuwajulia hali baadhi ya wagonjwa wa Kijiji cha Mchangani, Kijiji cha Ndijani Nyamiza na Unguja Ukuu katika wilaya ya Kati wakati wilaya ya Kusini alitembelea Kijiji cha Pete, Mzuri Makunduchi, na Bwejuu ikiwa ni siku ya pili ya ziara yake.




Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman , akisalimiana na Mohammed Khatib Maulid wa Kijiji cha Unguja Ukuu ambae ni mgonjwa aliyevunjika mguu kutokana na ajali aliyoipata mwanzoni mwa mwaka huu, wakati Othman alipofika nyumbani kwake kumjulia hali. **PICHA NA MPIGA PICHA WETU**

# Rais Mwinyi aeleza fursa za mashindano, kusoma Qur'an

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa kufanya mashindano ya kuhifadhi na kusoma Qur'an katika Mwezi Mtukufu wa Ramadhan ni fursa nyingine ya ibada na fadhila za kusoma Qur'an katika mwezi huo.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo katika Masjid Zenjbar Mazizini Unguja, katika fainali ya mashindano ya kimataifa ya kuhifadhi Qur'an yaliyozishirikisha nchi mbalimbali katika Bara la Afrika.

Katika hotuba yake, alieleza kwamba Uislamu unahimiza katika Mwezi wa Ramadhani kufanyike jitihada katika kusoma Qur'an, na ndiyo mwezi ilioteremshwa katika usiku wa Laylatul Kadr.

Alieleza kuwa utaratibu wa mashindano ya kuhifadhi na kusoma Qur'an ni kuwaandaa Maulamaa na Masheikh wa baadae.

"Hili ni jambo jema linalojenga misingi mizuri ya dini kwa vijana tangu wangali na umri mdogo na kuwafanya wakue wakiwa wameandaliwa vyema katika maisha ya ucha Mungu na kufanya mambo ya kheri," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, aliipongeza na kuishukuru Jumuiya ya Kuhifadhisha Qur'an Zanzibar kwa kuwa mstari wa mbele katika kuliendeleza jambo hilo la kheri tokea kuanzishwa kwa jumuiya hiyo miaka 30 iliyopita.

Alitoa shukrani kwa Waislamu na wafadhili wote wanaohamasika kuchangia kwa namna moja au nyingine katika kuhakikisha mashindano ya kuhifadhi na kusoma Qur'an yanafanyika na kupata mafanikio kila mwaka.

Aliwapongeza wazazi kwa kuona umuhimu wa kuwasaidia vijana kushiriki katika mambo kama hayo ya kheri na kutoa shukran maalum kwa walimu na masheikh waliowaandaa kwa kuwasomesha vijana washiriki, hadi wakaweza kufikia hatua ya fainali ya mashindano ya mwaka huu.

Dk. Mwinyi alitoa wito kwa Waislamu wote kujenga utamaduni wa kuchangia masuala mbalimbali ya kuimarisha Uislamu ikiwamo kusaidia ujenzi wa madrasa, misikiti na vituo vya kiislamu.

Pia, alipokea ombi la jumuiya hiyo la kuwasaidia vijana waliohifadhi Juzuu 30 za Qur'an waliomaliza kidato cha sita ambao wana sifa za kuendelea katika masomo ya chuo kikuu ambao hawakupata ufadhili wa masomo yao atawaunga mkono kwa kuwasaidia kuwatafutia wadhamini.

Mufti Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Saleh Omar Kabi, alieleza umuhimu wa kuhifadhi Qur'an na kueleza imani aliyonayo kwa vijana hao ya kuuendeleza Uislamu katika nchi wanazotoka.

Amiri wa Jumuiya hiyo, Sheikh Suleiman Omar Ahmed, alisema matunda ya jumuiya hiyo yanaonekana kwa kuwezesha kuzalisha vijana wengi waliohifadhi Qur'an na nchi nyingi katika Bara la Afrika kujitokeza kushiriki katika mashindano hayo.

Mashindano hayo yaliwashirikisha wanafunzi 13 kutoka Zanzibar, Tanzania Bara, Kenya, Rwanda, Uganda, Burundi, Malawi, Niger, Msumbiji, Comoro, Nigeria na Chad, ambapo mshindi wa kwanza alikuwa Hussein Youssouf Adam kutoka Chad, wa pili Saidi Doushimana kutoka Rwanda, wa tatu ni Hassane Djibrilla Oumarou kutoka Niger na wa nne ni Muslim Salum Seif kutoka Zanzibar.

# 'Kilimo cha viungo, matunda, mboga fursa'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo, Shamata Shame Khamis, amesema utekelezaji mradi wa viungo , mboga na matunda Zanzibar unaisaidia serikali kufikia lengo lake la kuinua vipato na uchumi kwa wananchi wake.

Amesema unawasaidia kwa kujiingiza katika shughuli za uzalishaji mazao ya kilimo kupitia taaluma na uwezeshwaji ambao wakulima wanapata kwenye mradi huo.

Alitoa kauli wakati wa ziara yake ya kutembelea mashamba ya wakulima wanufaika wa mradi huo kisiwani Pemba unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU).

Alisema dhamira ya Serikali ya Zanzibar ni kutambua wadau wote wanaoisaidia kufikia malengo yake kupitia miradi ya maendeleo inayotekelezwa ili kujua ufanisi na uhalisia kwenye kuwanufaisha wananchi walengwa.

Akizungumza na wakulima katika Shehia ya Ole, Wilaya ya Chake Chake, mkoa wa Kusini Pemba, Waziri Shamata alipongeza hatua ambazo mradi wa viungo imezichukua kwa wakulima ili kuhakikisha lengo lake linafikiwa.

"Niwapongeze sana watekelezaji wa mradi huu wa viungo Zanzibar kwa juhudi zenu za kuendelea kutoa mchango wenu kuisaidia serikali kuinua uchumi wa wananchi kupitia kilimo," alisema na kuongeza:

"Huu ni mwelekeo mzuri kwenye sekta ya kilimo kupata miradi kama hii, na mimi nimekuja hapa na kaulimbiu yangu ya 'toka kijiweni tukutane shambani' kwa sababu huku shambani ndipo kwenye maneno sio vijiweni."

Katika kuhakikisha wakulima wanaondokana na changamoto za kitaalamu zinazowarejesha nyuma kiuzalishaji, Waziri huyo alimuagiza ofisa mdhamini wa wizara hiyo kupeleka jopo la watafiti wa udongo kwa wakulima wa nyanya Shehia ya Mjini Ole ili kubaini chanzo cha mazao yao kushambuliwa na wadudu waharibifu.

Alisisitiza watekelezaji mradi huo kuandaa mpango maalum wa kushajihisha jamii juu ya umuhimu wa kutumia matunda kwa wingi ili kuwezesha matunda hayo kupata soko zaidi na kuongeza lishe kwa wananchi.

"Nakuombeni watekelezaji wa mradi huu, tunafahamu wananchi wengi bado hawana utamaduni wa kutumia matunda, hivyo tuweke mkakati maalum wa kuhamasisha matumizi ya matunda hasa mapapai kwa wingi kwenye jamii ili kurahisisha upatikanaji wa masoko kwa mazao yanayozalishwa na hawa wakulima wetu," alisisitiza.

Malik Hamad Khamis, mkulima wa matunda mnufaika katika mradi huo kutoka Shehia ya Ole, Chake Chake Pemba, alisema uwapo wa mradi umemfungulia fursa ya kuwekeza katika kilimo hicho kutokana na taaluma ya uzalishaji bora wa mazao aliyopata kwenye mradi.

Naye Meneja uendeshaji wa mradi huo kanda ya Pemba, Sharif Maalim Hamad, alisema mradi unatumia mbinu za kuwashirikisha wakulima viongozi kwenye shehia ili kufikisha haraka elimu kwa wakulima.

Waziri alitembelea maeneo mbalimbali ya wakulima ambayo mradi wa viungo unatekelezwa ikiwemo mashamba ya matunda, viungo na mboga katika mikoa ya Kusini na Kaskazini Pemba ambapo pia alipata fursa ya kushudia jinsi wakulima hao wanatumia taaluma ya kilimo chenye kuzingatia mabadiliko ya tabianchi katika shughuli zao za uzalishaji.

Mradi wa viungo , mboga na matunda Zanzibar ni wa miaka minne ambao unatekelezwa Unguja na Pemba kwa ushirikiano wa taasisi za People's Development Forums (PDF), Community Forests Pemba (CFP) na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania, TAMWA Zanzibar kupitia mpango wa AGRICONNECT kwa ufadhili wa EU.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**CHRISTINA MWITA MARWA** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE375033 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam 2020 . Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu naye.

**POLISITAARIFA: DAR/MAG/RB/143429/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAYUNI W. KOPWE** anatangaza kupotelewa na cheti cha Diploma in Clinical Medicine chenye namba NS0107/0036/2015 cha **MACHAME HEALTH TRAINING INSTITUTE** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha **Polisi. Taarifa ya polisi: LUS/RB/522/2022.**

## DEED POLL
### THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT (CAP.117)



BY THIS DEED, I SAUMU OMARY SHEMSHUZA of P.O.BOX Dar es salaam originally known as **SAUMU HAMAD OMARY HERE BY** absolutely and utterly renounce and abandon the use of my said names and IN LIEU thereof DO ASSUME as from this date hereof the name of **SAUMU OMARY SHEMSHUZA.**

**AND** in pursuance of such change of name as aforesaid, I hereby declare that I shall at all times herafter in all actions and proceedings and in all dealings and transactions and upon all occasions whatsoever use and sign the name of **SAUMU OMARY SHEMSHUZA** as my name in lieu of the said name **SAUMU HAMAD OMARY** which I have renounced as aforesaid

**AND I HERE BY** expressly authorized and requests all person to designate and address me by the name of **SAUMU OMARY SHEMSHUZA**

**THAT** the reason for such change of name is due to that all documents are registered in the name of **SAUMU OMARY SHEMSHUZA**

I FURTHER DECLARE that my former names SAUMU HAMAD OMARY are the names as SAUMU OMARY SHEMSHUZA, hence all transactions, certificates deed and commitment that I have done in the past by using my former names are valid

**IN WITNESS WHEREOF** I have hereto subscribed my name of **SAUMU OMARY SHEMSHUZA** on the day and in the manner here in after appearing.

BEFORE ME:
COMMISSIONER FOR OATHS
DRAWN BY:
BETWARIYA LYIMO
ADVOCATE

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya MOROGORO**

**Kituo cha MJINI Mkoa Wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......2022**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU BARNABAS JOHN WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA ALEXANDAR ALEX MAPUNDA**

## TANGAZO

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 12 Mwezi 4 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yoyote mwenye wosia na marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia ya narehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.
- Marehemu hakuacha wosia
- Futa isiyohusika.

Imetolewa Tarehe 29 Mwezi 03 Mwaka 2022.

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
MAHAKAMA

Simu Nambari: +255(0)28 250 1044
Simu Nambari: +255 (0) 28 250 1045
Fax Na: 028 - 2500117
Unapojibu tafadhali taja:
Unapojibu tafadhali taja:

Ofisi ya Hakimu Mkazi Mfawidhi
Mahakama ya Mwanzo Mjini,
S.L.P. 155,
MWANZA.

Kumb. Na. MADAI NA 50/2022 06/04/2022

Afisa Masoko,
Ofisi ya Magazeti,
MWANZA

YAH: SHAURI LA MADAI NA 50/2022
MDAI:......................................TUJIJENGE TANZANIA LIMITED
DHIDI YA

WADAIWA 1. AMINA JOHN SABUHORO
2. FATUMA MAKARANI KUSALARILA

19 Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 08/04/2022 saa 2.00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani. Endapo hutafika Mahakamani shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA.

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA

216798802

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KHAMIS BAKARI JUMA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA RAV4** yenye namba za ya usajili **T934 CMN, CHASSIS NAMBA JTEHH20V600025113, ENGINE NAMBA 3SFE4561239.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI CONTROL NUMBER: 9910832598970**

## JOSINA COMPANY LIMITED & AUCTIONEER.

**DEBT COLLECTIONS & AUCTIONEERING**
**HEAD OFFICE –Buzuruga plaza 2nd Floor Room No. 207 Mwanza, Tarime, Geita, Musoma, Bukoba**
**P.O BOX 11126 MWANZA, 0713/0789/0768-203040, josinacompany@gmail.com,josinacoltd@gmail.com**

### TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kwa Amri tuliyopewa na Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya na mkoa wa Mwanza. **JOSINA COMPANY LIMITED,** Itaendesha mnada wa hadhara wa kuuza Kiwanja cha **BENAYA DAVID KAKOYO,** Kiwanja Na. 1085 Kitalu "F"Nyegezi,Jijini Mwanza lililopo katika Mtaa wa Majengo,Kata ya Mkolani.hii ni kutokana na shauri la maombi namba 84/2022. kati ya **OPENING FINANCING GROUP DHIDI YA BENAYA DAVID KAKOYO na LUDOVICK RINGIA.**

**Mnada huu utafanyika tarehe 14/04/2022, siku ya Alhamisi.**

**MASHARTI YA MNADA**

KIWANJA litauzwa kama lilivyo ,mnunuzi atalipia 25%ya bei yam nada papo hapo baada ya nyundo ya dalali na 75%italipwa ndani ya siku kumi na nne (14)toka siku ya mnada ,na akishindwa kulipa mnada utarudiwa na pesa iliyolipwa awali haitarudishwa.

Ukaguzi wa eneo kiwanja utaanza leo tarehe **11/03/2022.**

**Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia namba 0713203040**

116798102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

Simu Nambari: +255(0)28 250 1044
Simu Nambari: +255 (0) 28 250 1045
Fax Na: 028 - 2500117
Unapojibu tafadhali taja:
Unapojibu tafadhali taja:

Ofisi ya Hakimu Mkazi Mfawidhi
Mahakama ya Mwanzo Mjini,
S.L.P. 155,
**MWANZA.**

**Kumb. Na. MADAI NA 50/2022** **06/04/2022**

Afisa Masoko,
Ofisi ya Magazeti,
**MWANZA**

**YAH: SHAURI LA MADAI NA 50/2022**
**MDAI:......................................TUJIJENGE TANZANIA LIMITED**
**DHIDI YA**

**WADAIWA** **1. AMINA JOHN SABUHORO**
**2. FATUMA MAKARANI KUSALARILA**

19 Unaamriwa na Mahakama ya Mwanzo Mjini Mwanza kufika tarehe 08/04/2022 saa 2.00 asubuhi bila kukosa ili kujibu madai yaliyofunguliwa hapa Mahakamani. Endapo hutafika Mahakamani shauri litasikilizwa upande mmoja na kutolewa uamuzi bila wewe kuwepo.

..................
HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
**MWANZA.**

HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MWANZA

216798802

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676**

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB:
+255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0782253676

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharasma yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
*benki kwa maendeleo yako*

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## WARAKA MIZANIA KWA TAREHE 31.12.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | | Mwaka wa sasa 2021 | Mwaka uliopita 2020 |
|---|---|---|---|
| **A.** | **MALI** | | |
| 1 | Fedha Taslimu | 13,193 | 11,959 |
| 2 | Salio Katika Benki Kuu ya Tanzania | 13,046 | 13,900 |
| 3 | Uwekezaji Katika Amana za Serikali | 41,088 | 22,770 |
| 4 | Salio Katika Benki Nyingine na Taasisi za Fedha | 479 | 17,178 |
| 5 | Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 61 | 40 |
| 6 | Miamala Baina ya Matawi | 14 | 26 |
| 7 | Bili Zilizoafikiwa | 0 | 0 |
| 8 | Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0 | 0 |
| 9 | Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 0 | 0 |
| 10 | Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0 | 0 |
| 11 | Mikopo Halisi Iliyopo | 77,709 | 77,703 |
| 12 | Mali Nyingine | 18,220 | 11,310 |
| 13 | Uwekezaji wa Hisa | 39 | 39 |
| 14 | Akaunti za udhamini | 0 | 0 |
| 15 | Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 15,076 | 14,813 |
| **16** | **JUMLA YA MALI** | **178,924** | **169,739** |
| **B.** | **DHIMA** | | |
| 17 | Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 756 | 1,511 |
| 18 | Amana za Wateja | 121,897 | 118,304 |
| 19 | Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| 20 | Amana Maalumu | 35 | 0 |
| 21 | Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0 | 0 |
| 22 | Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0 | 1 |
| 23 | Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 3,091 | 3,075 |
| 24 | Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0 | 0 |
| 25 | Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0 | 0 |
| 26 | Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazoli | 8,246 | 8,192 |
| 27 | Dhima Nyingine | 10,044 | 9,478 |
| 28 | Madeni | 5,980 | 713 |
| **29** | **JUMLA YA DHIMA** | **150,051** | **141,274** |
| **30** | **MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29)* | **28,874** | **28,465** |
| **C.** | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| 31 | Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 27,797 | 10,984 |
| 32 | Akiba ya Mtaji | 0 | 0 |
| 33 | Mapato Yaliyobakizwa | (12,101) | (5,627) |
| 34 | Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 0 | 0 |
| 35 | Akaunti Nyingine za Mtaji | 13,177 | 23,108 |
| 36 | Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0 | 0 |
| **37** | **JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **28,874** | **28,465** |
| 38 | Dhima Zisizo Dhahiri | 111 | 102 |
| 39 | Mikopo Chechefu | 13,191 | 11,924 |
| 40 | Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 6,214 | 6,927 |
| 41 | Mali Nyingine Chechefu | 73 | 73 |
| **D.** | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| (i) | Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 16.1% | 16.8% |
| (ii) | Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 15.7% | 12.6% |
| (iii) | Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 67.4% | 69.4% |
| (iv) | Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 83.8% | 83.2% |
| (v) | Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 66.4% | 59.2% |
| (vi) | Ongezeko la Amana | 2.1% | 8.5% |
| (vii) | Ongezeko la Mali | 5.4% | 0.2% |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI
## KWA MWAKA UNAOISHIA 31.12.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Limbikizo la Mwaka wa sasa 2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 2020 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 25,427 | 24,890 |
| 2 Gharama za Riba | (8,092) | (7,804) |
| 3 **Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **17,335** | **17,087** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0 | 0 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | (2,249) | (4,405) |
| 6 **Mapato Yasiyo ya Riba**: | **4,529** | **4,174** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 240 | 286 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 3,654 | 3,227 |
| 6.3 Gawio | 0 | 0 |
| 6.4 Mapato Mengine | 636 | 661 |
| 7 **Gharama Zisizo za Riba:** | **(25,094)** | **(25,156)** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | (14,123) | (13,057) |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 0 | 0 |
| 7.3 Gharama Nyingine | (10,971) | (12,099) |
| 8 **Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **(5,479)** | **(8,301)** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 0 | (1,617) |
| 10 **Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **(5,479)** | **(9,918)** |
| 11 Mapato Mengine Yaliyojumuishwa (bainisha) | 0 | 1 |
| 12 **Jumla ya Faida (Hasara) iliyojumuishwa kwa mwaka** | **(5,479)** | **(9,917)** |
| 13 Idadi ya Waajiriwa | 406 | 418 |
| 14 Mapato kwa Hisa | (197) | (903) |
| 15 **Idadi ya Matawi** | **18** | **18** |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (i) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | -3.2% | -5.9% |
| (ii) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | -19.1% | -39.8% |
| (iii) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 109.3% | 115.3% |
| (iv) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 12.8% | 12.9% |

## TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA
## KWA MWAKA ULIOISHIA 31.12.2021
(Kiasi kwa shilingi milioni)

| | Limbikizo la Mwaka wa sasa 2021 | Limbikizo la Mwaka Linganishi 2020 |
|---|---|---|
| **I: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uendeshaji:** | | |
| Mapato/(Hasara) Halisi | (5,479) | (8,301) |
| Marekebisho kwa Ajili ya: | | |
| - Hasara Katika Mali | 5,524 | 7,630 |
| - Badiliko Halisi Katika Mikopo | (2,483) | 2,086 |
| - Faida/Hasara Kwenye Mauzo ya Mali | (22) | 0 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana | 2,604 | 9,874 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Amana za Muda Mfupi Zilizoafikiwa | (18,305) | 2,680 |
| - Mabadiliko Halisi Katika Dhima Nyingine | (323) | 351 |
| -Mabadiliko Halisi Katika Mali Nyingine | 4,576 | (10,855) |
| - Kodi Iliyolipwa | (124) | (1,877) |
| - Mengineyo (bainisha) | 955 | 1,704 |
| ***Fedha Halisi zilizotolewa (zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji*** | **(13,078)** | **3,292** |
| **II: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Uwekezaji:** | | |
| Gawio Lililopokewa | 0 | 0 |
| Ununuzi wa Mali za Kudumu | (365) | (133) |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Mali za Kudumu | 22 | (19) |
| Ununuzi wa Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Mauzo ya Amana Zisizoshughulikiwa na Mawakala | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | 0 | 0 |
| ***Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Uwekezaji*** | **(344)** | **(152)** |
| **III: Mtiririko wa Fedha Kutokana na Shughuli za Kifedha:** | | |
| Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0 | 0 |
| Mapato Kutokana na Utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0 | 16,992 |
| Gawio Lililolipwa kwa Fedha Taslimu | 0 | 0 |
| Mabadiliko Halisi Katika Madeni Mengine | 0 | 0 |
| Mengineyo (bainisha) | (2,442) | (2,497) |
| **Fedha Halisi Zilizotolewa (zilizotumika) kwa Shughuli za Kifedha** | **(2,442)** | **14,495** |
| **IV: Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu:** | | |
| Ongezeko / Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | (15,864) | 17,635 |
| Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa Robo Mwaka/Mwaka | 36,259 | 18,624 |
| **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa Robo Mwaka/Mwaka** | **20,395** | **36,259** |

## AKIBA COMMERCIAL BANK PLC
## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31.12.2021

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya Kisheria | Tengo la Ziada ya Jumla | Mengineyo | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2021** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(5,626,989)** | **3,683,694** | **-** | **16,992,072** | **28,465,109** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (5,479,466) | 0 | 0 | 0 | **(5,479,466)** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Miamala na wanahisa | 16,813,000 | 0 | 179,072 | 0 | 0 | (16,992,072) | **0** |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (1,173,519) | 1,173,519 | 0 | 0 | **0** |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mengineyo (Tangulizi la mtaji wa Hisa) | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 5,888,000 | **5,888,000** |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2021** | **27,797,416** | **2,431,917** | **(12,100,902)** | **4,857,213** | **-** | **5,888,000** | **28,873,644** |
| **Mwaka Uliopita** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka 01.01.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **4,687,639** | **3,286,944** | **0** | **0** | **21,390,916** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | 0 | 0 | (9,917,878) | 0 | 0 | 0 | (9,917,878) |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Miamala na wanahisa | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Ziada ya Kisheria | 0 | 0 | (396,750) | 396,750 | 0 | 0 | 0 |
| Tengo la Ziada ya Jumla | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mengineyo | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 16,992,072 | 16,992,072 |
| **Salio la mwisho wa mwaka 31.12.2020** | **10,984,416** | **2,431,917** | **(5,626,989)** | **3,683,694** | **0** | **16,992,072** | **28,465,109** |

## BAADHI YA MAELEZO KWA MWAKA UNAYOISHIA 31.12.2021

Sisi, tuliotajwa hapo chini, wajumbe wa bodi ya wakurugenzi, tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu, tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi, na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006, na zinaonesha hali halisi.

| Jina | Saini | Tarehe |
|---|---|---|
| 1. Ernest Massawe | | |
| 2. Prof. Josephat Lotto | | |



# SARE SIMBA CHEREKO YANGA

**Na Adam Fungamwango**

OFISA Habari wa Klabu ya Yanga amesema watani zao wa jadi, Simba kwa sasa wamebaki na dua la kuku, kuombea wao wapoteze mechi ili waweze kutetea ubingwa wao, kitu ambacho ni kigumu mno.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Bumbuli alisema baada ya suluhu ambayo Simba iliipata dhidi ya Polisi Tanzania juzi kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro, kumekuwa na pengo la pointi 10 na sasa kinachoendelea ni wapinzani wao kuomba dua la kuku ili wapoteze mechi na si vinginevyo, kwani hata wakishinda mechi zote hawawezi kuwakuta.

"Nawaambia kuwa hizi pointi 10, ambao tumewapita waendelee tu kuomba dua la kuku ambalo siku zote halimpati mwewe, na hivi tuko kwenye mikakati ya kuliongeza pengo kwa sababu tarehe 30 tutaifanya hiyo kazi ya kuongeza pengo, kwa hiyo nawataka wanachama na mashabiki wa Yanga wajae tu mapema uwanjani, kwa sababu hii ni mechi yetu, sisi ndiyo wenyeji, tena kama watafungwa, watakuja na mawenge ya kutolewa Afrika Kusini ndiyo kabisa," alisema Bumbuli.

**Simba na Yanga zitacheza mechi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Aprili 30, mwaka huu siku sita baada ya Simba kumaliza kucheza mechi ya marudiano ya robo fainali ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Orlando Pirates ya Afrika Kusini Aprili 24.**

Kuhusu mechi ya robo fainali ya Kombe la FA dhidi ya Geita Gold, Bumbuli aliwashukuru makocha na wachezaji wa timu hiyo kwa kupambana kwani mechi ilikuwa ngumu, kiasi kwamba ililazimika kwenda kwenye mikwaju ya penalti.

Yanga imetinga hatua ya nusu fainali, ambapo inasubiri mshindi kati ya Simba dhidi ya Pamba.

Kwa maana hiyo huenda msimu huu kukashuhudiwa mechi tatu za watani wa jadi, Simba na Yanga.

**MILIKI...**



Kiungo wa Simba, Rally Bwalya akimiliki mpira dhidi ya beki wa kati wa Polisi Tanzania, Mohamed Mmanga kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Ushirika mjini Moshi, Kilimanjaro juzi na kumalizika kwa sare tasa. **PICHA: SIMBA**

# Ben Pol ageukia changamoto za kijamii

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa muziki wa R&B, Bernard Paul 'Ben Pol', amesema mbali na muziki sasa ameamua kuendelea kutumia sauti na jina lake katika kusaidia utatuzi wa changamoto mbalimbali zinazoikumba jamii.

Akizungumza na mwandishi wetu jana, Ben Pol alisema sasa anashiriki katika kampeni ya siku 16 za kupinga ukatili wa kijinsia inayofanyika kila mwaka na kwamba kwa kushirikiana na ubalozi wa Ufaransa walifanya tamasha jijini Dar es Salaam Desemba mwaka 2021.

"Mimi ni Shujaa niliyeteuliwa na Umoja wa Mataifa (UN), kwa ajili ya kutoa hamasa juu ya malengo ya maendeleo endelevu (SDGs). Ni Balozi wa mazingira kupitia wizara ya nchi ofisi ya makamu wa raisi muungano na mazingira.

"Balozi wa Justdiggit taasisi ya kimataifa yenye mlengo wa kuifanya Afrika kuwa kijani kwa kutumia njia asilia kwa kushirikiana na Lead foundation. Balozi wa WildAid inayoshughulika na uhifadhi wa wanyamapori na kupinga ujangili," alisema.

Alisema katika shughuli za kijamii, anafanya kazi kwa karibu na Shirika la WWF ambapo hivi karibuni wamefanya wimbo unaoitwa Africa Song for Nature.

Ben Pol, alisema pia alichaguliwa kuwakilisha Afrika Mashabiki katika World Youth Forum 2022, jukwaa kubwa zaidi la vijana duniani linalofanyika kila mwaka nchini Misri na kukutanisha vijana kujadili utatuzi wa masuala mbalimbali yanayoikumba dunia.

Aidha, alisema siku chache zilizopita ameachia wimbo mpya unaoitwa 'Twa Dance' alioshirikiana na Dallah, ambao unapatikana katika mitandao yote ya muziki na media zote, na sasa yupo jikoni kuandaa albamu mpya anayotarajia kuizindua Septemba mwaka huu.

Alisema katika albamu hiyo itashirikisha miamba ya muziki kutoka pembe zote za Afrika.

## Ligi Kuu Wanawake Z'bar kuendelea Mei

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Wanawake mzunguko wa lala salama unatarajiwa kuendelea mapema Mei 10, mwaka huu baada ya kukamilika mfungo wa Mwezi wa Ramadhani.

Ligi hiyo katika mzunguko huu wa pili, itachezwa katika vituo viwili vya Unguja na Pemba ikilingamishwa na raundi ya kwanza ambapo ilichezwa kituo kimoja cha Unguja pekee.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Soka la Wanawake (ZFF), Hawa Abdallah Ally, alisema katika mzunguko wa pili, timu zilizopo Unguja zitazifuata zile za Pemba kwenda kucheza nao.

Alisema hatua hiyo ni kutokana na Pemba kuwa na timu chache, hivyo kila mzunguko timu mbili za Unguja zitakwenda kucheza Kisiwani Pemba kwa michezo yao ya ugenini na nyumbani.

"Mzunguko wa pili tunatarajia kucheza Pemba na Unguja. Mzunguko huu ndio tunaenda kumpata bingwa wa ligi Kuu ya Wnawake msimu huu wa 2021-2022," alisema.

Ligi Kuu ya Wanawake Zanzibar inajumla ya timu 10 ambapo timu ya Warriors Queens ndio kinara wa ligi hiyo ikiwa imevuna alama 27 ikifuatiwa na New Generation yenye pointi24 na nafasi ya tatu inashikwa na Green Queens yenye alama 18.

## Taifa Kuogelea yaelekea Zambia

**Na Saada Akida**

TIMU ya Taifa ya Kuogelea ya Tanzania, imeondoka leo kuelekea Zambia kwenye mashindano ya Kanda ya Nne, yanayotarajiwa kuanza kutimua vumbi Aprili14 hadi 18, mwaka huu, mjini Lusaka nchini humo.

Akizungumza na gazeti hili wakati wa kukabidhi bendera kwa timu hiyo, Katibu Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa, (BMT), Neema Msitha, aliitaka kuhakikisha wanaipeperusha vema bendera ya Tanzania katika mashindano hayo.

Alisema serikali itashirikiana na Chama cha Kuogelea nchini(TSA), kuhakikisha mchezo huo unapiga hatua na baadaye kuleta medali katika mashindano mbalimbali ikiwamo hiyo ya Kanda ya Nne.

"Mnakwenda kuuwakilisha umma wa mamilioni ya Watanzania, fanyeni jitihada za kuhakikisha mnafanya vizuri na tunatarajia mataleta medali ya michezo hiyo ya Kanda ya Nne," alisema Neema.

Naye Mwenyekiti wa TSA, Imani Alimanya, alisema waogeleaji 18, kuanzia umri wa miaka 11 na zaidi ndio walitarajiwa kuondoka leo, kuelekea katika mashindano hayo.

## ZISIKUPITE

### LUKAKU ATAKIWA PSG
KLABU ya Paris St-Germain wanahusishwa katika mazungumzo ya kusaini mkataba na mshambuliaji wa Chelsea, Romelu Lukaku mwaka mmoja tu baada ya mchezaji huyo wa Kimataifa wa Ubelgiji mwenye umri wa miaka 28, kuwagharimu 'Blues' pauni milioni 98 kutoka Inter Milan. ***(But via Sun)***

### LEIPZIG WAMTAKA HAG
RB Leipzig wanajaribu kutaka kumchukua kocha anayetajwa kutua Manchester United, Erik ten Hag kutoka Ajax. (***Telegraph***)

### NUNEZ AWINDWA ARSENAL
KLABU za Manchester United na Arsenal zimejiunga na mbio za kumsaka Darwin Nunez baada ya kutuma ujumbe wao kumfuatilia mshambuliaji wa Uruguay mwenye umri wa miaka 22, ambaye kwa sasa anachezea Klabu ya Benfica. (***Mirror***)

### LUIZ ATAKIWA ROMA
AS Roma wanataka kusajili kiungo wa kati wa Aston Villa, Mbrazil Douglas Luiz, mwenye umri wa miaka 23, msimu huu. ***(Calciomercato)***

### HAALAND HAITAKI UNITED
MSHAMBULIAJI wa Borussia Dortmund, Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21 amepuuzilia mbali nia ya kujiunga na Klabu ya Manchester United kwa sababu mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway haamini kuwa wanaweza kutimiza matamanio yake ya ndani ya uwanja. (***ESPN***)

### LINGARD AGOMBEWA ULAYA
AS Roma, AC Milan na Juventus wamejiunga na West Ham pamoja na Newcastle katika kuelezea nia yao ya kumuwania mshambuliaji Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 29, wakati mkataba wake kule Manchester United ukimalizika msimu huu. ***(Mirror)***

### HAZARD HUYOOO DOTRMUND
KLABU ya Borussia Dortmund ndio inayopendelewa katika kumsajili mshambuliaji Mbelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 31 kutoka Real Madrid - na katika mbio hizo wako mbele ya Arsenal na AC Milan. (***Cadena Ser)***

### UNITED KUPANGA SAFU
KLABU ya Manchester United inapanga kukamilisha kupanga safu yake ya kati msimu huu, huku kiungo wa kati Mfaransa mwenye umri wa miaka 29, Paul Pogba akitarajiwa kuondoka wakati mkataba wake utakapoisha Juni mwaka huu. ***(Mirror)***

### GVARDIOL AOTA MBAWA
FURSA ya Tottenham ya kusaini mkataba na mlinzi Mcroatia, Josko Gvardiol msimu huu "huenda isifanikiwe kabisa" huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20, akisema anafurahia kuwapo katika klabu ya Ujerumani ya RB Leipzig. (***RB Live***)

### COLWILL LULU ULAYA
KLABU kadhaa za Ligi Kuu England na Ulaya, zinatarajiwa kuchukua hatua ya kumsajili beki, Levi Colwill mwenye umri wa miaka 19, ambaye anacheza mchezo wa kufurahisha akiwa na mkataba wa mkopo kule Huddersfield msimu huu. (***Fabrizio Romano***)

### ASENSIO KUONDOKA MADRID
NYOTA wa Hispania, Marco Asensio anatarajia kuondoka Real Madrid msimu huu huku AC Milan na Tottenham zikiwa na nia na nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 . (***Mundo Deportivo)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA: MAN CITY INAHITAJI TAJI LA UEFA

**Hakuna namna yoyote ya kuwa timu kubwa Ulaya bila kubeba ubingwa Ligi ya Mabingwa, kwani...**

**MANCHESTER,** ENGLAND

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amekubali kuwa timu yake inapaswa kuchukua ubingwa wa Ligi ya mabingwa Ulaya kabla ya kutambulika kama moja ya klabu kubwa barani Ulaya.

Man City pamoja na uwekezaji wote uliofanywa kwenye klabu hiyo, lakini bado haijafanikiwa kuchukua ubingwa wa Ulaya.

Guardiola amesema Man City haiwezi kuwekwa pamoja na klabu kubwa Ulaya kama Barcelona, Manchester United, Real Madrid na nyingine kubwa kama haijachukua ubingwa wa ulaya.

**"Nakubaliana na watu am bao waanasema kuwa hatu jafanikiwa Ulaya, hatu jashinda ubingwa wa Ulaya huenda wako sahihi," alise ma Guardiola akinukuliwa na BBC Sport.**

"Ili kutambulika na kila mtu nje ya Ulaya na duniani ni kutawala soka la Ulaya," aliongeza Guardiola ambaye timu yake ilitoka sare ya kufungana bao 2-2 na Liverpool Jumapili.

"Hakuna namna yoyote ya kuwa timu kubwa Ulaya bila kuwa na taji la Ligi ya Mabingwa, kwani hapo ndio kwenye kipimo kikubwa kwako."

Kikosi hicho cha Guardiola sasa kimeipita pointi moja Liverpool kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu England.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 1,144

MECHI KALI
REAL MADRID
VERSUS
CHELSEA
1 | 2.44
X | 3.27
2 | 2.82

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# SPURS, ARSENAL KWA ASENSIO

**LONDON,** England

KLABU ya Tottenham Hotspur ni miongoni mwa timu ambazo zimefanya mawasilioni na wakala wa Marco Asensio kuhusu uwezekano wa kupata saini yake kwenye majira ya joto wakati huu Klabu ya Real Madrid wakitarajia kumuweka sokoni mwishoni mwa msimu huu.

Asensio hadi sasa ameichezea klabu hiyo michezo 26 huku akiwa ameanza kwenye mechi 15 msimu huu.

Japokuwa kuna sintofahamu kati yake na Klabu ya Madrid na kusababisha kuwekwa sokoni mwishoni mwa msimu.

Mkataba wa Asensio na Madrid unamalizika mwaka 2023, mpaka sasa amekataa kusaini mpya ambao klabu hiyo imemuandalia, ndio maana wanataka kumuweka sokoni mwishoni mwa msimu ili kuweza kupata fedha na kuzui kumpoteza bure baada ya msimu huu kuisha na wako tayari kusikiliza ofa inayoanzia pauni milioni 30.

Kwa mujibu wa taarifa zilizopo ni klabu mbili tu mpaka sasa kutoka England ambazo zimefanya mawasiliano na wakala wa Asensio kuhusu kupata huduma yake ambazo ni Tottenham na Arsenal.



## Hag kutua Utd wakati wowote

**MANCHESTER,** England

TAARIFA kutoka Manchester United zinaeleza klabu hiyo ipo kwenye hatua za mwisho kukamilisha mchakato wa kumtangaza Erik Ten Hag kuwa kocha mkuu akitokea Ajax ya Uholanzi.

Kocha huyo ataanza majukumu msimu ujao akitoka katika orodha ya makocha waliokuwa wakipewa nafasi kubwa ya kuajiriwa, wengine wakiwa ni Mauricio Pochettino wa PSG, Luis Enrique (Timu ya Taifa ya Hispania) na Julen Lopetegui (Sevilla).

Ten Hag mwenye umri wa miaka 52, atachukua nafasi ya Ralf Rangnick ambaye ni kocha wa muda, aliyepewa nafasi hiyo baada ya United kumfukuza Ole Gunnar Solskjaer mwaka jana.

Kwa muda mrefu Man United ilikuwa ikitajwa kumuwania kocha huyo kwa ajili ya kuwanoa 'Mashetani Wekundu' hao ambao wamekuwa na msimu mbaya.

Jumamosi Man United walikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Everton kwenye mchezo wa Ligi Kuu England.

Man United kwa msimu huu itamaliza bila taji lolote na pia ina uwezekano wa kushindwa kufuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao.

## HABARI MICHEZO




# 4,195,580

# JACKPOT
## MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 16/04/2022 | 17:00 | Watford vs Brentford | 2.66 | 3.16 | 2.66 |
| 02. 16/04/2022 | 17:15 | Alaves vs Rayo Vallecano | 2.57 | 3.03 | 2.93 |
| 03. 16/04/2022 | 17:30 | Manchester City vs Liverpool | 2.35 | 3.21 | 2.96 |
| 04. 16/04/2022 | 18:00 | St Etienne vs Brest | 2.31 | 3.21 | 3.11 |
| 05. 16/04/2022 | 20:00 | Dijon vs AC Ajaccio | 2.31 | 3.10 | 3.15 |
| 06. 16/04/2022 | 20:00 | Nimes vs Sochaux | 2.44 | 3.15 | 2.90 |
| 07. 16/04/2022 | 20:00 | Valenciennes vs Le Havre | 2.65 | 3.15 | 2.65 |
| 08. 17/04/2022 | 16:00 | Metz vs Clermont Foot | 2.65 | 3.15 | 2.70 |
| 09. 17/04/2022 | 16:15 | Newcastle vs Leicester | 2.50 | 3.20 | 2.80 |
| 10. 17/04/2022 | 18:30 | Union Berlin vs Eintracht Frankfurt | 2.38 | 3.26 | 2.91 |
| 11. 17/04/2022 | 20:30 | Bayer Leverkusen vs RB Leipzig | 2.71 | 3.41 | 2.46 |
| 12. 17/04/2022 | 20:30 | Giresunspor vs Besiktas | 2.88 | 3.28 | 2.36 |
| 13. 17/04/2022 | 22:00 | Sevilla FC vs Real Madrid | 3.19 | 3.19 | 2.31 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMANNE - 12/04/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 1869 | FC Noravank vs Van Yerevan | 2.44 | 2.83 | 2.97 |
| 13:00 | 4653 | Cagliari Youth vs Torino Youth | 2.15 | 3.45 | 3.20 |
| 14:00 | 1368 | Adelaide Comets vs Adelaide Olympic | 1.74 | 4.00 | 4.10 |
| 14:00 | 5401 | Bristol City U23 vs Ipswich U23 | 2.00 | 3.59 | 3.11 |
| 15:00 | 4525 | Addis Ababa City FC vs Mekelakeya | 2.43 | 2.77 | 3.06 |
| 15:30 | 4352 | Inter Youth vs Napoli Youth | 1.33 | 5.05 | 6.61 |
| 16:00 | 1879 | Orgryte IS U21 vs BK Hacken | 7.00 | 5.64 | 1.28 |
| 16:00 | 2010 | Uganda Revenue Authority FC vs Vipers SC | 3.54 | 2.91 | 2.11 |
| 16:00 | 2682 | Mamelodi Sundowns vs Golden Arrows | 1.22 | 5.54 | 12.86 |
| 16:00 | 3435 | Busoga United vs FC Saints | 2.38 | 2.82 | 3.07 |
| 16:00 | 3538 | Urartu vs Artsakh | 2.08 | 2.87 | 3.69 |
| 16:00 | 3728 | Mbarara FC vs Police FC (UGA) | 2.53 | 2.87 | 2.82 |
| 17:00 | 3123 | FK CSKA 1948 II vs Hebar Pazardzhik | 2.23 | 2.97 | 3.17 |
| 17:00 | 5958 | Osters IF U21 vs Halmstads BK U21 | 3.70 | 4.00 | 1.72 |
| 17:45 | 2208 | Ol. Medea vs CS Constantine | 3.65 | 2.87 | 2.09 |
| 17:45 | 2275 | NA Hussein Dey vs WA Tlemcen | 1.54 | 3.44 | 6.21 |
| 17:45 | 4492 | RC Arbaa vs MC Magra | 2.34 | 2.67 | 3.35 |
| 18:00 | 2957 | Sokol Sieniawa vs MKS Czarni Polaniec | 1.84 | 3.50 | 3.70 |
| 18:00 | 3570 | Kuressaare vs Flora Tallinn | 14.58 | 7.77 | 1.11 |
| 18:00 | 4546 | Spal Youth vs AC Milan Youth | 3.65 | 3.70 | 1.91 |
| 18:00 | 5029 | Sebeta City FC vs Ethiopia Bunna SC | 3.45 | 2.82 | 2.20 |
| 18:00 | 5195 | Norrby IF vs Varbergs Bois U21 | 3.74 | 4.08 | 1.70 |
| 18:45 | 3775 | Saipa Karadj vs Shahrdari Astara | 2.01 | 3.05 | 4.10 |
| 18:45 | 4125 | Rayka Babol vs Ghasghaei Shiraz | 2.46 | 2.60 | 3.55 |
| 19:00 | 2859 | Shahrdari Hamedan vs Pars Jonoubi Jam | 2.75 | 2.65 | 3.05 |
| 19:00 | 3140 | Slavia Sofia vs CSKA Sofia | 4.56 | 3.25 | 1.75 |
| 19:00 | 3449 | Malavan Bandar Anzali vs Esteghlal Khuzestan | 1.79 | 3.20 | 5.20 |
| 19:00 | 4383 | Machine Sazi Tabriz vs Mes Shahr-e Babak | 5.80 | 3.05 | 1.76 |
| 19:00 | 4659 | Hermanstadt vs Universitatea Cluj | 2.29 | 2.92 | 3.12 |
| 19:00 | 5043 | Shams Azar Qazvin vs Khosheh Talaei | 2.90 | 2.75 | 2.75 |
| 19:00 | 5049 | Shahin Bushehr vs Vista Turbine | 5.60 | 2.70 | 1.91 |
| 20:00 | 1474 | Orebro SK vs Jonkopings Sodra | 2.01 | 3.47 | 3.63 |
| 20:00 | 4167 | TSG Balingen vs SV Elversberg | 8.00 | 4.88 | 1.30 |
| 20:00 | 4462 | SV Kirschanschoering vs VFB Hallbergmoos | 1.32 | 4.87 | 7.41 |
| 20:30 | 4618 | Baroka FC vs Orlando Pirates | 4.47 | 2.83 | 1.99 |
| 21:00 | 1891 | Kosovo W vs Belgium W | 38.83 | 15.53 | 1.01 |
| 21:00 | 4377 | Maritzburg Utd vs Moroka Swallows FC | 2.05 | 2.68 | 4.56 |
| 21:45 | 1164 | Biggleswade Town vs Coalville Town | 3.11 | 4.08 | 1.88 |
| 21:45 | 1324 | Kettering Town vs Guiseley | 1.56 | 3.83 | 5.04 |
| 21:45 | 1326 | Burton vs Wigan | 3.82 | 3.37 | 1.92 |
| 21:45 | 2012 | Longford Town vs Cobh Ramblers | 1.49 | 4.09 | 5.45 |
| 21:45 | 2693 | Chorley vs York City | 2.28 | 3.15 | 2.91 |
| 21:45 | 4035 | Lowestoft Town vs Stourbridge | 3.40 | 4.10 | 1.87 |
| 21:45 | 4087 | Southport vs Leamington | 1.72 | 3.50 | 4.28 |
| 21:45 | 4679 | Taunton Town vs Yate Town | 1.68 | 4.07 | 3.88 |
| 21:45 | 5090 | Bognor Regis vs Cheshunt | 3.05 | 4.10 | 2.00 |
| 21:45 | 5660 | Portsmouth vs Rotherham | 2.77 | 3.17 | 2.48 |
| 22:00 | 2254 | Real Madrid vs Chelsea | 2.44 | 3.27 | 2.82 |
| 22:00 | 2409 | Bayern Munchen vs Villarreal | 1.24 | 6.17 | 9.56 |
| 22:30 | 5686 | Zamalek vs Farco FC | 1.48 | 4.18 | 6.17 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# NYOTA WA TEMBO WARRIORS ATUPIA HAT-TRICK LIGI UTURUKI

**Na Saada Akida**

MSHAMBULIAJI wa timu ya Taifa ya Tanzania ya Watu wenye Ulemavu, 'Tembo Warriors', Alfani Kiyanga, anayecheza soka la kulipwa katika Klabu ya Yeditepe ya Uturuki, amefunga mabao matatu 'hat-trick' na kuisaidia timu hiyo kushinda katika mchezo wa Ligi Kuu ya Watu wenye Ulemavu nchini humo.

Yeditepe juzi iliibuka na ushindi wa mabao 3-0 dhidi ya ODTU, yote yakifungwa na Kiyanga huku bao moja akifunga kwa msaada mkubwa kutoka kwa Mtanzania mwenzake anayekipiga katika klabu hiyo, Shedrack Hebron, ambaye alimmegea pasi ya mwisho (assist).

**Kiyanga amesajiliwa mwezi uliopita na mechi ya juzi ilikuwa mchezo wake wa pili tangu amesaini mkataba wa miaka miwili kuichezea klabu hiyo, mechi ya kwanza akitengeneza nafasi na juzi alifanikiwa kufunga hat-trick yake ya kwanza tangu kujiunga na klabu hiyo.**

Baada ya matokeo hayo, Rais wa Shirikisho la Mpira wa Miguu kwa Watu wenye Ulemavu nchini (TAFF), Peter Sarungi, alisema mwenendo wa wachezaji hao ni ishara nzuri kwa Tembo Warriors ambayo inajiandaa kushiriki Kombe la Dunia baadaye mwaka huu.

"Kufanya vizuri kwa wachezaji wetu katika klabu wanazotumikia ni ishara kubwa kwa timu yetu ya Taifa (Tembo Warriors), inayojiandaa na Kombe la Dunia kwa kuwa wachezaji hao wanafanya vizuri huko na kuja kusaidia hapo baadaye katika michuano hiyo," alisema Sarungi.

Alisema kwa kiwango wanachoendelea kuonyesha wachezaji hao, TAFF inajivunia mafanikio hayo na inaendelea kutafuta fursa kwa wachezaji wengine wa ndani kwenda kucheza soka la kulipwa ili baadaye kuwa msaada kwa Tembo Warriors.



Simba Queens. **PICHA: MAKTABA**

# Simba Queens bila Olpa mwendo mdundo

**Na Adam Fungamwango**

IKICHEZA bila straika wake tegemeo, Olpa Clement, timu ya soka ya Wanawake ya Simba, Simba Queens, juzi iliendeleza ushindi wake wa asilimia mia moja kwenye Ligi Kuu ya Wanawake, ilipoichapa Ruvuma Queens mabao 2-0 kwenye Uwanja wa Majimaji mjini Songea mkoani Ruvuma.

Yalikuwa ni mabao ya Asha Djaffar raia wa Burundi dakika ya 12, na Mtanzania Amina Ramadhani dakika ya 14, yaliyotosha kuwapa ushindi huo, wakati Simba Queens ikiendelea kujiweka kwenye mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa kwa mara nyingine tena.

Olpa kwa sasa yupo nchini Uturuki, alikokwenda kufanya majaribio ya kucheza soka la kulipwa.

Simba Queens inaendelea kuwa kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo, ikicheza mechi 13, na kushinda zote, mabao 62 ya kufunga, ikiruhusu nyavu zake kutikiswa mara nne tu ikiwa imefikisha pointi 39.

Kwenye mechi zingine za Ligi Kuu Wanawake nchini, zilizochezwa juzi, Mlandizi Queens ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani wa Mabatini mkoani Pwani, iliivurumisha Alliance Girls mabao 3-1, huku Oysterbay Queens ikiichapa JKT Queens mabao 4-2 kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Leo katika Uwanja wa Uhuru, Yanga Princess, ambayo nayo ikiwa haina straika wake tegemeo aliyekwenda kucheza soka la kulipwa nchini Sweden, Aisha Masaka, itashuka dimbani kucheza dhidi ya Baobab.

# Michezo

Jumanne Aprili 12, 2022

Nipashe




Guardiola: City inahitaji taji Uefa UKURASA 21

HESABU NYINGI...



Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akipiga hesabu ya kumtoka beki wa pembeni wa Geita Gold FC, Amos Charles kwenye mechi ya robo fainali ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na Yanga kushinda kwa mikwaju ya penalti 7-6 baada ya sare ya bao 1-1 ndani ya dakika 90. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Simba mapema tu kuiwinda Orlando

**Na Adam Fungamwango**

HAKUNA kulala! Hivyo ndivyo unavyoweza kusema baada ya wawakilishi pekee wa Tanzania kwenye michuano ya kimataifa kwa ngazi ya klabu, Simba kumaliza mechi ya Ligi Kuu Bara mjini Moshi juzi na moja kwa moja kwenda kukwea pipa kurejea Dar es Salaam kuingia kambini tayari kuiwinda Orlando Pirates ya Afrika Kusini.

Simba ambayo juzi iliambulia sare tasa dhidi ya Polisi Tanzania kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Ushirikia, Moshi mkoani Kilimanjaro, Jumapili wiki hii itaikaribisha Orlando Pirates kwenye mechi ya robo fainali ya kwanza ya Kombe la Shirikisho Afrika itakayopigwa Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza baada ya kuwasili kwenye Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, Meneja Habari na Mawasiliano wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kuwa ni kweli wamepata matokeo yasiyoridhisha, lakini akawataka wanachama na mashabiki wa timu hiyo kutotumia muda mwingi kujadili kilichopotea, badala yake kupigania kile kilicho mbele yao.

"Si matokeo ya kufurahisha hata kidogo, lakini tunapaswa kuyasahau haraka na akili yetu sasa tuielekeze kwenye jambo kubwa lililo mbele yetu robo fainali ya Afrika Jumapili dhidi ya Orlando Pirates.

Najua tumeumizwa na matokeo haya, lakini hatuna budi kuyapokea na kuheshimu juhudi za wapinzania wetu, Polisi Tanzania kwa sababu walikuwa bora nyumbani kwao, walicheza kwa 'jihad' na kwao sare hiyo imewatosha na kuwafurahisha.

"Wenye akili timamu hawatumii muda mwingi kujadili kilichopotea, badala yake ni kuwekeza nguvu kupigania kilicho mbele yetu," alisema Ahmed.

Kuhusu kuachwa kwa tofauti ya pointi 10 na vinara wa Ligi Kuu, Yanga alikiri kuwa pengo ni kubwa, lakini bado hawajakata tamaa na watapigana hadi mwisho kuangalia watakapokuwa wamefikia.

"Mbio ni ngumu, lazima ukubali kuwa alama 10 ni nyingi, lakini hilo halitutishi na sisi tunazidi kupambana, tumebakiwa na mechi 11 mbele, ikifika mwisho wa ligi tutaangalia tumevuna nini."

# Yanga yawalilia Aucho, Fei Toto

**Na Saada Akida**

## ●●● Ni baada ya Geita Gold FC kuwaonyesha pengo lao, kocha asema bila nyota hao timu haitembei mbele...

BAADA ya kufanikiwa kutinga kwa mbinde nusu fainali ya Kombe la Shirikisho la Azam (ASFC), maarufu FA Cup juzi, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, amesema pamoja na mafanikio hayo kutokuwapo kwa Feisal Salum 'Fei Toto' na Khalid Aucho ni tatizo kubwa kwao katika utengenezaji wa nafasi.

**Yanga juzi ilifuzu nusu fainali ya Kombe la FA kwa mikwaju ya penalti 7-6 baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Geita Gold FC kwenye mechi ya robo fainali iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.**

Akizungumzia mchezo huo baada ya mechi kumalizika, Kaze alisema mchezo ulikuwa mgumu kwa upande wao kutokana na wachezaji kucheza kwa kupooza na Geita Gold FC kumiliki vizuri mpira hasa katika safu ya kiungo na kushindwa kutengeneza nafasi ya mabao.

Alisema Fiston Mayele na Saido Ntibazonkiza hawakuwa fiti kwa asilimia 100, hivyo kusababisha kucheza chini ya kiwango na hayo yote yakichangiwa na kukosekana kwa mtu wa kupelekea mipira.

"Tatizo si kufunga au kutumia washambuliaji wawili, bali lilikuwa ni kukosekana kwa mtu wa kufikisha mipira mbele, tumeliona hilo na sasa tutalifanyia kazi kwa kipindi hiki ambacho tutawakosa Fei Toto na Aucho," alisema na kuongeza:

"Mechi ilikuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu Geita Gold FC walicheza vizuri dakika zote walifika mbele na kupata nafasi moja na kuitumia vizuri, sisi tulishindwa [redacted] ka hatua ya penalti na bahati kuwa kwetu," alisema Kaze.

Kuhusu suala la kipa wao, Djigui Diarra kukosa penalti, ilikuwa bahati mbaya kwa sababu kipa huyo ni mzuri na hufanya vizuri katika mazoezi ya kupiga penalti.

"Tunashukuru kupita na kwenda kucheza nusu fainali na sasa tunaenda kujiandaa na michezo yetu ijayo kwa kufanyia kazi mapungufu yetu," alisema Kaze.

Kwa uapnde wa Kocha Mkuu wa Geita Gold FC, Fred Felix Minziro, alisema alikuja kutafuta matokeo, lakini mwisho wa siku Yanga walifanikiwa kupita kwa Penalti.

"Tumekubali matokeo bahati haikuwa kwetu, Yanga wamefanikiwa kushinda na sasa tunaangalia mechi zilizopo mbele yetu kwa kufanyia kazi mapungufu yetu," [redacted]

Naye mchambuzi wa soka, Ally Mayai alisema kutokuwapo kwa Fei Toto na Aucho kunaonyesha mapungufu katika safu ya kiungo ya Yanga ndiyo sababu iliwafanya Geita kutawala kati.

"Yanga walishindwa kupata watu ambao wanapelekea mipira mbele, kwa sababu ukiangalia Geita Gold FC walifanikiwa kutawala nafasi ya kiungo na kuhakikisha Yanga wanashindwa kupeleka mipira mbele," alisema.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >